# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## Kikao cha Arobaini na Nne – Tarehe 10 Juni, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali Waheshimiwa Wabunge na tunaanza na maswali kwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake, kwa niaba yake.

Na. 564

### Mitaji kwa Vijana Wanaomaliza Vyuo vya Ufundi Nchini

**MHE. STELLA S. FIYAO K.n.y. MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza: -

Je, Serikali inawasaidiaje vijana wanaomaliza *VETA* na vyuo vingine vya ufundi kupata mitaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi nchini tangu kuanza utekelezaji wake mwaka 2016/2017, imewezesha jumla vijana 101,579 kupata mafunzo kwa njia ya uanagenzi. Mafunzo hayo yamekuwa yakifanyika kupitia vyuo mbalimbali vya ufundi vya Serikali na binafsi ambavyo vimewezesha vijana kupata mafunzo ya ufugaji wa viumbe maji kupitia taasisi za Serikali na binafsi na kuwawezesha vijana kupata mafunzo ya unenepeshaji mifugo kupitia taasisi za Serikali na binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya vijana 101,579 walionufaika na mafunzo ya uanagenzi, vikundi vya vijana 219 vyenye jumla ya vijana 1,621 vimewezeshwa vifaa mtaji kwa ajili ya kuendeleza ujuzi walioupata. Vikundi vya vijana 118 vyenye vijana 1,008 vimewezeshwa cherehani 372, vikundi vya vijana 56 vyenye vijana 369 vimewezeshwa vifaa vya uchomeleaji seti 65 na vikundi 45 vyenye vijana 58 vimewezeshwa vifaa vya kutengeneza bidhaa za *aluminium* seti 58, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Fiyao.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri bado kuna kundi kubwa la vijana hasa vijijini ambao bado hawajanufaika na fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue mkakati wa Serikali kuhakikisha vijana wote waliopata mafunzo wananufaika na fursa ya kupewa mitaji? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**10 JUNI, 2024**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI:)** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella Fiyao kwa niaba ya Mheshimiwa Tunza Malapo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imeweka programu mbalimbali kwa vijana kuweza kunufaika kulingana na makundi, lakini pia kwa hali zao na kwa taaluma zao. Wale vijana ambao wapo vijijini wananufaika kupitia halmashauri katika fedha zinazotengwa na Serikali za mapato ghafi 10% na 4% kwenda kwa ajili ya vijana katika maeneo hayo wanayokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ipo mifumo mingine ya kuwagusa vijana walio vijijini walio kwenye taaluma wanapata fedha kupitia bodi ya mikopo na Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametenga zaidi ya shilingi bilioni 734 ambazo zitawanufaisha hata wale wanaotoka kijijini, lakini hivyo hivyo kwenye Wizara ya Michezo umeona wanasanaa wamekuwa wanapewa zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuwezeshwa kama mikopo na *start up capital* kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya kilimo hivyo hivyo *BBT* chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa uratibu na usimamizi na utekelezaji Wizara ya Kilimo vijana zaidi ya 812 na vijana 700 ambao wameenda mpaka JKT umeendelea kupewa na kunufaika na fedha hizi za Serikali, hivi juzi utaona katika *BBT life* chini ya Wizara ya Uvuvi na Mifugo, vijana wa mfano zaidi ya 300 pale Mwanza walihitimu, lakini katika Serikali na nchi nzima tunategemea vijana zaidi ya 10,000 kunufaika kwenye programu hiyo ambapo tayari Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametenga shilingi bilioni 10.3 zitakazoenda kuwanufaisha vijana watakaoingia kwenye unenepeshaji mifugo, lakini pia ufugaji wa Samaki na kufanya shughuli za viumbe maji kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kijana wa Kitanzania ambaye ataachwa kwenye programu hizi za Serikali hadi kwenye madini ipo programu maalumu iliyoanzishwa sasa hivi ya *Mining*

*for Brighter Tomorrow* ambayo nayo pia tunaenda kwa vijana wale walio kwenye sekta ya madini kuwasaidia waweze kuchimba lakini pia kupata vifaa na mikopo saidizi na kupunguza masharti ili kila mmoja aweze kunufaika katika ujenzi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo la Mheshimiwa Rais limenyooka kwamba kwa vijana wote ndiyo nguvu kazi ya Taifa zaidi ya 34.5%, lakini pia ni nguvu kazi 57% lazima tuitumie kikamilifu kuweza kuhakikisha wanashiriki katika ujenzi wa Taifa lao na kushiriki kwenye masuala ya uongozi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunahamia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 565

**Hitaji la Walimu wa Sayansi Meatu**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuongeza walimu wa sayansi katika shule za sekondari Wilaya ya Meatu?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiajiri walimu wa masomo mbalimbali wakiwemo wa masomo ya sayansi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi mwaka 2022/2023 Serikali iliajiri walimu wa masomo ya sayansi 8,425 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Meatu ilipata walimu 113 wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023/2024 Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 wa masomo mbalimbali wakiwemo wa sayansi ambao watapangiwa vituo vya kazi katika maeneo yenye upungufu mkubwa ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Meatu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Mkoa wa Simiyu una upungufu mkubwa sana wa walimu, walimu wa sayansi na walimu wa *arts*. Walimu waliopo ni 861 kwa shule hizo 31, lakini pungufu ni walimu 844 kwa mkoa mzima wa Simiyu, je, ni lini Serikali italeta walimu hao ili kukidhi mahitaji wa elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna shule 30 katika Mkoa wa Simiyu ambazo hazina kabisa walimu wa kike na walimu wa kike ni muhimu sana kuwa katika shule kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike mahitaji yao, je, ni lini sasa Serikali italeta walimu wa kike katika shule hizo 30 ambazo hazina walimu wa kike?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuwasemea watoto na hasa kwenye masuala ya kupata elimu iliyo bora, lakini kuhusiana na swali lake la kwanza kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi kwamba mwaka huu 2023/2024 Serikali inatarajia kuajiri walimu 12,000 wa masomo mbalimbali ikiwemo wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mgao na yeye katika mkoa wake watapata mgao wa walimu na tutaweza kupunguza ukali wa upungufu wa walimu katika Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili ambalo Mheshimiwa Mbunge ametaka kupata uhakika wa kupata walimu wa kike, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika walimu 12,000 ambao tutatarajia kuajiri katika mwaka huu tutazingatia na tutaweka kipaumbele cha upatikanaji wa walimu wa kike na hasa katika shule za mkoa wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Shule ya Sekondari ya Tingirima ni mpya na haina mwalimu wa kike hata mmoja, Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kujua hivi hakuna utaratibu wa kuchukua walimu popote pale katika shule za Bunda ukapeleka maeneo yale badala ya kusubiri hao walimu wa ajira? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali inaajiri walimu kwa ajili ya kupunguza upungufu wa walimu, lakini hatua nyingine ambayo inachukuliwa na Serikali ni kuhakikisha inafanya msawazo ili kupunguza walimu ambao wapo kwenye shule nyingine ambao wamerundikana wapo wengi kuwapunguza kwenye maeneo ambayo yana upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua hiyo pia Serikali inaichukua katika kupunguza ukali wa upungufu wa walimu katika shule na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalitazama hili suala la shule yake hii kwa upekee kabisa ili tuweze kuchukua hatua hizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata. Swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, litaulizwa na Mheshimiwa Margaret Sitta. Litaulizwa na Mheshimiwa Ngassa.

Na. 566

**Hitaji la Fedha Ujenzi wa Kituo cha Afya Igusule – Bukene**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA K.n.y. MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa Kituo cha Afya Igusule – Bukene?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 Serikali ilipeleka shilingi bilioni moja katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Magengati na Itobo. Vituo hivi vimekamilika na vinatoa huduma. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Nzega itatenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Igusule na Serikali kuu itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa kituo hicho, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, kwa kuwa tathimini inaonesha vituo vingi vya afya vya kata vinajengwa kati ya shilingi milioni 500 mpaka milioni 700 na kwa kuwa hii shilingi milioni 100 iliyotengwa kwa mapato ya ndani haitajosha, je, ipi *commitment* ya Serikali kuhusu wananchi wa Igusule kwenye Jimbo la Bukene?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwenye Jimbo la Igunga Kata ya Kining'inila pia Serikali ilituahidi kupeleka shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha kimkakati kitakachohudumia Kata za Isakamaliwa, Mbutu, Kining'inila na

Mwamashimba, je, majibu ya Serikali ni yapi kwa kuwa imekuwa ni muda mrefu toka tuahidiwe kwamba tutapata fedha kutoka Benki ya Dunia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa ujenzi wa vituo vya afya Serikali iliweka mpango wa kujenga vituo hivi kwa awamu. Tunajenga kwa awamu ya kwanza kwa kupeleka fedha kati ya shilingi milioni 500 hadi shilingi milioni 700 kutoka Serikali Kuu lakini pia Serikali ilitoa maelekezo kwa ajili ya halmashauri kutenga mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati wakati Serikali ikitafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge uwe na uhakika tu kwamba hii shilingi milioni 100 inatoka mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi na Serikali Kuu itapeleka fedha nyingine kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo kwa kadri ya mahitaji yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kuhusiana na kituo cha afya katika kata ya kimkakati ya Jimbo hilo la Igunga, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu ulishawasilisha Ofisi ya Rais – TAMISEMI na sisi tumeshaingiza kwenye orodha ya vituo vya kimkakati mara fedha ikishapatikana tutahakikisha tunapeleka ili kituo hicho cha afya kiweze kujengwa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Zanzui, Wilaya ya Maswa ina wakazi wengi, je, ni lini Serikali itatuletea fedha tujenge kituo cha afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Kata ya Zanzui tayari imeshaainishwa kama ni kata ya kimkakati kwa maana ya kukidhi vigezo vya idadi ya wananchi, umbali kutoka kituo cha jirani zaidi, nichukue nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Maswa kuwasilisha rasmi taarifa hiyo Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kuingiza kwenye mpango, lakini kama ilishaingizwa kwenye mpango basi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha na tuna uhakika baada ya mwaka huu wa fedha vituo vingi vya kimkakati vitaanza kujengwa ili kupeleka huduma za afya karibu na wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Susuni na Kata ya Mwema iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Tarime wanatembea umbali mrefu sana kufuata huduma ya afya Sirari au Tarime Mjini, ni lini Serikali itawajengea vituo vya afya kwenye kata hizi kwa sababu wamekidhi vigezo vyote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hiyo ya Mwema na Susuni katika Jimbo la Tarime Vijijini ni miongoni mwa kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia mara kwa mara na mimi tu nikuhakikishie kwamba tumeshaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri kuainisha maeneo yoyote ya kata za kimkakati yenye uhitaji mkubwa wa vituo vya

afya na kuanza kutenga fedha za mapato ya ndani kupitia 60% au 40% ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime Vijijini kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo hivyo katika maeneo hayo kwa awamu wakati Serikali ikitafuta fedha kwa ajili ya kuunga mkono na kukamilisha vituo hivyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujua na kuiuliza Serikali kwamba Kituo cha Afya cha Ntuntu katika Jimbo la Singida Mashariki kilitengewa shilingi milioni 500 huu unaenda ni mwaka wa pili hakijaanza kazi pamoja kuwa tulipata fedha kwa awamu mbili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua sasa ni lini kituo cha afya kitaanza kazi kwa sababu wananchi wanakisubiri kwa muda mrefu na ni kituo cha kimkakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya vituo vya afya ambavyo vilijengwa na vimekamilika, lakini bado havijaanza kutoa huduma. Naomba nitumie nafasi hii kuwakumbusha na kuwasisitiza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kikiwemo Kituo hiki cha Afya cha Ntuntu katika Jimbo la Singida Mashariki kwamba vituo hivi baada ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kupeleka fedha baada ya kukamilika matarajio ya wananchi ni kuanza kupata huduma za afya katika vituo hivyo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haitakuwa tayari kuona kuna kituo cha afya kimekamilika lakini hakitoi huduma na wananchi wanahitaji huduma. Mheshimiwa Mbunge mimi nitumie nafasi hii nimpe maelekezo Mkurugenzi wa Singida kuhakikisha

ndani ya miezi miwili kituo kinaanza kutoa huduma na wananchi wanaanza kupata huduma katika kituo hicho, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya TAMISEMI ilitaka kila jimbo liainishe kituo cha afya cha kimkakati katika kila kata, je, ni lini Serikali itatoa fedha ikiwemo kituo cha afya ambacho kipo katika Kata ya Lyabukande, Shinyanga Vijijini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kujali afya za wananchi ilianzisha mpango wa ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati katika kata zenye sifa hizo na tayari Mheshimiwa Rais ametoa fedha kwa ajili kujenga vituo vya afya zaidi ya 878 mpaka sasa. Mpango huu ni endelevu ikiwemo kata ambayo Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava ameitaja tutahakikisha tunaingiza kwenye mpango mkakati wa kujenga kwa awamu ili tuweze kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Shamsia, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha katika Kata ya Mkunwa kwa ajili ya kumalizia kituo cha afya kilichopo katika halmashauri yetu ya wilaya ili wananchi waweze kufurahia huduma hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vituo vya afya ambavyo vimepewa shilingi milioni 250 vinasubiri shilingi milioni 250 kwa ajili ya ukamilishaji na vituo hivyo vyote vimeshawekwa kwenye mpango wa awamu ya pili ya ukamilishaji wa shilingi milioni 500.

Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu kituo hicho kilipata shilingi milioni 250, tunafahamu kwamba majengo hayajakamilika kwa mahitaji yanayotakiwa na tayari tumeshaweka mpango kwa ajili ya kumalizia shilingi milioni 250 kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo hicho cha afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ighondo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona na naomba kuuliza; ni lini sasa Serikali italeta fedha kukamilisha boma la afya Kituo cha Ngimu ambalo wananchi wamelijenga miaka 14 sasa na limekuwa likiahidiwa muda mrefu bila ahadi hiyo kukamilika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Ighondo Ramadhani, kwanza niwapongeze wananchi wa Kata hiyo ya Ngimu kwa kujenga hicho kituo cha afya ambacho hakijakamilika na dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vituo hivyo vinakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kituo hicho kimejengwa kwa miaka 14 na mpaka sasa hakijakamilika na ikiwa ni kipaumbele cha Serikali ni wajibu wa Mkurugenzi na Menejimenti yake kuhakikisha wanatoa kipaumbele katika bajeti zao angalau kwanza kukamilisha kituo hicho cha afya na baadaye kuomba fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya umaliziaji.

Kwa hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo aone umuhimu kama boma limekaa kwa miaka 14 maana yake pia kunakosekana *commitment* ya Mkurugenzi, ni lazima waingize kwenye menejimenti watenge bajeti za mapato ya ndani na kuanza ujenzi wakati wanafuatailia kupata fedha za Serikali Kuu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regina Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Eshkesh, Wilaya ya Mbulu Vijijini wamekuwa wakitembea umbali mrefu sana kufuata huduma za afya. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka kituo cha afya katika Kata hii ya Eshkesh? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, safari ni hatua na tumeshaanza, tumeshapeleka fedha katika Halmashauri ya Mbulu kwa ajili ya vituo kadhaa vya afya, zahanativ lakini pia fedha kwa ajili ya vifaa tiba. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba zoezi la ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati ikiwemo kwenye hii Kata ya Eshkesh ni endelevu na tutatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga kituo hicho cha afya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata linahusu pia afya mnaweza mkaendelea kusimama. Swali la Mheshimiwa Khadija Shabani Taya, Mbunge wa Viti Maalum litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Neema Mgaya.

Na. 567

**Upungufu wa Watumishi Vituo vya Afya na Zahanati Nchini**

**MHE. NEEMA W. MGAYA K.n.y. MHE. KHADIJA S. TAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itashughulikia tatizo la upungufu wa watumishi kwenye vituo vya afya na zahanati nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa changamoto ya upungufu wa watumishi wa sekta ya afya katika vituo vya kutolea huduma. Hivyo, Serikali imeendelea kuajiri wataalamu wa kada mbalimbali za afya ambapo katika kipindi cha miaka mitatu (2021, 2022 na 2023), Serikali imeajiri jumla ya watumishi 18,418 wa kada mbalimbali za afya na kuwapangia vituo kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2024/2025 Serikali inatarajia kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya 10,112 ambapo baada ya taratibu za ajira kukamilika watapangwa kwenye vituo vyenye upungufu mkubwa wa watumishi kote nchini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Neema Mgaya, maswali ya nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mbunge mwenye swali la msingi ni Mbunge ambaye anawakilisha kundi la watu wenye ulemavu angependa kujua katika vituo hivyo vya afya na zahanati hizo Serikali imezingatia vipi utoaji wa vifaa kinga vya watu wenye matatizo ya Ngozi/watu wenye ulemavu wa ualbino?

Swali la pili, mwakilishi wa wananchi wa watu wenye ulemavu pia angependa kujua kwamba Serikali imejenga vituo vya afya vipya na imezingatia miundombinu ya watu wenye ulemavu; je, ni lini Serikali itaenda kuboresha miundombinu ili kuweza kukidhi watu wenye ulemavu kwenye vituo vya afya na zahanati zilizojengwa zamani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka kipaumbele cha hali ya juu sana katika kuwawezesha watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali wakiwemo watu wenye ulemavu wa ngozi kwa maana ya albino na katika bajeti za Serikali kupitia fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya lakini mapato ya ndani ya vituo imewekwa kabisa eneo au kanuni ya kutenga fedha kwa ajili ya kununua mafuta ya kuwagawia watu wenye changamoto za afya ya ngozi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili linafanyika na Serikali imekuwa ikifuatilia kuona kwamba fedha inayotengwa inapelekwa kwa albino wanaopatikana katika maeneo hayo ili kuwakinga na mionzi ya jua, na zoezi hili ni endelevu tutaendelea kufanya kila mwaka wa bajeti kuhakikisha wananchi hawa wanapata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na miundombinu wezeshi kwa watu wenye ulemavu, ni kweli kwamba Serikali imeweka kipaumbele hicho na katika ujenzi wa miundombinu yote ya huduma za afya tumeweka maeneo ambayo yanawawezesha watu wenye ulemavu kuweza kupita na viti mwendo au kwa namna nyingine kwa urahisi zaidi. Pia tumehakikisha maeneo ya vyoo yanakuwa na vyoo ambavyo ni vya walemavu na maeneo mengine yote, na nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kusimamia hilo ili watu wenye ulemavu wapate huduma katika mazingira yaliyobora zaidi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mwaka 2021 wakati wa ziara ya Makamu wa Rais akiwa kule Newala, Serikali ilisema kwamba itatuletea mtaalamu wa *ultrasound* katika Kituo cha Mkwedo ambacho kipo Jimbo la

Newala Vijijini, lakini mpaka leo mtaalamu huyo hajaletwa. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ile? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tulishaweka mpango wa kumpeleka mtaalam wa *ultrasound* katika Kituo cha Afya cha Mkwedu na alishapangiwa kwa bahati mbaya alipata changamoto. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumesha-*allocate* mtumishi mwingine kwa ajili ya kwenda kuchukua nafasi ya yule ambaye alipangiwa na hakuweza kufika ili wananchi wa Mkwedu waweze kupata huduma za *ultrasound*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwa kuwa Serikali ilishafanya sensa na kuwatambua watu wenye ulemavu wote waliopo ndani ya nchi hii, sasa je, Serikali haioni haja wale walemavu hasa wa ngozi wapelekewe mafuta yao kulingana na idadi iliyopo badala ya kusubiri mpaka bajeti itolewe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali imetambua idadi ya watu wenye ulemavu na hususan *albino* kwa muktadha huu na katika kila bajeti ya kituo na katika bajeti ya halmashauri, msingi wa kutenga bajeti ni idadi ya watu wenye ulemavu katika eneo hilo kwamba wanatambuliwa katika kata husika, katika kijiji husika wako wangapi na dawa zile za kukinga ngozi zinapelekwa kwenye zahanati kulingana na idadi ya watu katika eneo hilo au kwenye kituo cha afya au kwenye hospitali ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kuboresha ili kuhakikisha

kwamba watu wenye ulemavu wote wanapata huduma hiyo ili kuwakinga na mionzi ya jua, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, wakati mwingine maelekezo ama ikama ya watumishi kwenye vituo vya afya na zahanati haiangalii uhalisia, kwa mfano Kituo cha Afya cha Kwenda, licha ya ikama kutimia bado kuna *volume* kubwa ya wagonjwa na licha ya hiyo ikama uya watumishi, ni mkakati gani wa kuongeza madaktari na ma-*nurse* kwenye hicho kituo kwa kuwa kina watu wengi sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kigezo cha ikama kutumika kama kigezo namba moja cha kupeleka watumishi katika ngazi ya huduma kwa maana ya zahanati, kituo cha afya au hospitali ya halmashauri, lakini pia tunaangalia hali halisi. Kuna vituo vya afya ambavyo vina idadi ndogo zaidi ya wananchi wanaopata huduma, lakini kuna vituo vya afya vya ngazi ile ile au zahanati ambavyo vina idadi kubwa sana ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge hicho Kituo cha Afya cha Kwenda ambacho umetupa taarifa tutaichukua tuone namna gani tunaongeza watumishi wa sekta ya afya pale ili waweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, maeneo ya pembeni kama Kilindi, Lushoto, Mkinga na Korogwe Vijijini kwenye Mkoa wa Tanga yanakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi wa afya kwenye zahanati na

vituo vya afya. Ni upi mkakati wa makusudi wa Serikali wa kuokoa maisha ya akina mama na watoto katika maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hakika ameweka mkakati wa makusudi kabisa wa kupunguza upungufu wa watumishi wa sekta ya afya katika vituo na ndio maana ndani ya miaka hii mitatu Serikali imeajiri watumishi zaidi ya 18,000 na watumishi hawa wanaajiriwa kupitia mfumo wa TEHAMA ambao umeweka nafasi nyingi zaidi katika maeneo ya pembezoni katika mikoa ya pembezoni yenye upungufu mkubwa zaidi ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kila ajira inapojitokeza watumishi walio wengi wanapelekwa maeneo ya pembezoni zaidi kwa sababu kule kuna upungufu mkubwa zaidi wa watumishi wa sekta ya afya. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata hizi ajira ambazo zinafuata tutahakikisha maeneo yale ya Kilindi na maeneo mengine yote ya pembezoni yenye upungufu mkubwa zaidi yanapewa kipaumbele cha watumishi ili kuweza kuboresha huduma katika maeneo hayo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona, lakini nilikuomba kwa swali linalofuata, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunahamia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, sasa aulize swali lake.

Na. 568

**Ukataji Holela wa Miti**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatunga sheria kali ya kuzuia ukataji miti holela hasa kwenye maeneo yenye milima na miinuko ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzuia ukataji holela wa miti katika maeneo ya milimani na miinuko, Serikali imetunga na inasimamia utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali. Sheria hizi ni pamoja na Sheria ya Mazingira, Sura 191, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 na Sheria ya Misitu, Sura 323, sheria zote hizi zina vifungu mahususi kuhusu uhifadhi na utunzaji wa mazingira na ulinzi wa milima, vilima na miinuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, sambamba na kutunga sheria, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha mazingira ya nchi yetu yanalindwa na kuhifadhiwa vizuri. Hatua hizo ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka 2006 unaoweka lengo la kila wilaya kupanda miti isiyopungua 1,500,000 kila mwaka na Mkakati wa Taifa wa Kupanda na Kutunza Miti wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza jitihada za uhifadhi katika maeneo ya milima na miinuko, Ofisi ya Makamu wa Rais

itashirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS),* Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mtaa na sekta binafsi katika kutoa elimu na kusimamia sheria zilizopo kwa sasa, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Moja, shughuli za kibinadamu zinazoendelea kandokando ya Bwawa la Mtera zimesababisha sana kuua mazalia ya samaki. Je, ni lini sasa Serikali itatoa kauli kali kabisa ya kuzuia kazi za kilimo zisiendelee kando kando ya bwawa hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimepokea malalamiko hapa kutoka kwa Madiwani wangu wawili, mmoja anaitwa Philemon Temaigwe na mwingine anaitwa Rukwakwa Nziku kwamba misitu yao na milima yao inakwisha, inavamiwa, vibali vinatolewa hovyo kukatakata misitu katika milima hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa haraka kutamka na kutoa zuio kazi hizi za kukata miti kwenye milima zisiendelee? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kiswaga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa kwa kuwa moja miongoni mwa vinara madhubuti sana kwenye jambo la uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli shughuli za kibinadamu zimekuwa zinachangia kwa kiasi kikubwa katika kuharibu na

kuchafua vyanzo vya maji. Sasa kupitia sheria yetu hii ya meta 60 tayari tumeshatoa maelekezo, lakini hatua nyingine ambayo tumeifanya ni kuhakikisha kwamba tunaendeleza kupanda miti ya kutosha maeneo yaliyozunguka vyanzo vya maji, lakini pia kuchukua hatua za kisheria kwa wale wote ambao wanachafua na kuharibu vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka nitoe wito kwa Watanzania wote, ni marufuku kufanya shughuli zozote za kibinadamu pasipo kuzingatia sheria ya meta 60 kwenye vyanzo vya maji, kuna watu mpaka kesho wanachepua maji, wanayatoa kutoka njia yao ya asili na wanapeleka kwenye njia isiyokuwa ya kawaida kwa sababu ya shughuli zao za kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanafanya shughuli za kilimo, shughuli za ujenzi, shughuli za makazi karibu na vyanzo hivi vya maji, mwisho wa siku wanaharibu mazingira, wanaharibu ikolojia ambayo inapatikana ndani ya maji. Kwa hiyo, Serikali inatoa kauli ni marufuku kufanya shughuli zozote za kibinadamu karibu ama kwenye vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika suala lingine la kuhakikisha kwamba tuna hifadhi na tunatunza maeneo haya ya milima, waambie Waheshimiwa Madiwani kwamba Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan ipo imara na ipo makini katika jambo la kuhifadhi na kutunza mazingira hasa maeneo haya ya miinuko, vilima na milima. Kwanza tunaenda kuongeza kupanda miti ya kutosha sana na hapa tunataka tuwaambie wananchi waongeze kupanda miti maeneo haya ya vilima, milima na miinuko ili tutunze mazingira sambamba na kusimamia sheria na kutoa elimu kwa wananchi, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Sasa Serikali pamoja na sheria kali ambazo mnataka kutunga hamwoni sasa ni wakati wa lile neno la kusema kata mti, panda mti limepitwa na wakati na iwe ni panda mti, tunza mti mwingine tuachane na ile kata mti panda mti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hilo jambo tumekaa na limo kwenye mipango yetu na ndiyo maana tumeanzisha kampeni nyingi sana za kupanda miti. Moja ni kampeni ya kusoma na mti ambayo tunawataka wanafunzi wote wa vyuo vikuu, wa sekondari, msingi na vyuo na Watanzania wote wahakikishe kwamba wanapanda miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukasema kupanda miti haitoshi, tuhakikishe kwamba baada ya miti kupandwa watu wanaishughulikia miti yao. Tunataka tutoe wito kama Serikali, kila anayepanda mti ashughulikie mti wake ili lengo na madhumini tutunze na tuhifadhi mazingira na miti ikue na tufikie lengo la kupanda miti hii, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anakiri kwamba kuna ukataji wa miti hovyo na kwa kuwa nchi yetu kinara wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi ni Mheshimiwa Rais. Ni upi mkakati wa Wizara wa kupanda mti kwa kutumia mbegu za asili, kuna maeneo mengi ya mapori ya asili yamepotea hasa ukienda huko Kusini lakini mataifa kama Kenya na Gambia wanafanya *aerial seeding* kwa kumwaga mbegu za asili kipitia *helicopter* au *drones.*

Ni upi mkakati wa Wizara kupambana na hilo kwa sababu kupanda mti mmoja mmoja imekuwa ikichukua nafasi ndefu na muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri alioutoa Mheshimiwa tunauchukua na tunakwenda kuufanyia kazi, ingawa tayari tulishafikiria hilo jambo kwa sababu tumeiona *speed* ya upandaji miti, mti mmoja mmoja, kwa hiyo mpaka tusubiri matukio kwa sababu Watanzania tumekuwa na utamaduni mpaka Siku ya Wanawake, uje Mwenge, sijui kuwe kuna Mapinduzi, kuna Muungano, sasa tumehisi kuna *distance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huo mpango ambao umeupendekeza tunakwenda kuufanyia kazi na *soon* tutaanza kuona utekelezaji wake, *Inshallah. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, maeneo mengi ya Tarafa ya Kilolo ni maeneo ya miinuko na yana misitu mingi inayopandwa na wananchi kwa hiyari yao. Haya maeneo ambayo miti inapandwa na wananchi kwa hiyari yao, je, Serikali ina mpango gani wa kutoa motisha kwa wananchi hawa ili waendelee kuwa na morali ya kupanda miti na kuitunza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli moja miongoni mwa ajenda kubwa ya Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan katika suala zima la utunzaji na uhifadhi wa mazingira, pamoja na mambo mengine ya utunzaji wa vyanzo vya maji, lakini tumesema la mwanzo tuhakikishe kwamba tunapanda miti

ya kutosha ili lengo na madhumuni tukipanda miti mambo mengine yatakuja, maana hata tukipanda miti hii kampeni ya *clean cooking* itapata nafasi, tunza vyanzo vya maji itapata nafasi na mambo mengine yatapata nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa ni kwamba moja miongoni mwa jambo ambalo tumelichukua kama sehemu ya hatua ni kuendelea kuelimisha wananchi juu ya suala zima la upandaji miti, umuhimu wa upandaji miti, umuhimu wa uwepo wa miti katika jamii na umuhimu wa uwepo wa miti katika kutunza na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwambie Mheshimiwa Mbunge tutakachokifanya, pamoja na yeye tushirikiane na wananchi na Watanzania wote kuelimisha wananchi kupanda miti kwa wingi, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa Mkoa wa Kagera wananchi wengi tumekuwa tukipanda miti kwa ajili ya kutunza mazingira na biashara, lakini kuna baadhi ya wananchi wakisafisha mashamba, wanachoma moto. Ningependa kujua, je, Serikali imetoa elimu kiasi gani ili wananchi wasichome moto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kupitia shughuli mbalimbali za kibinadamu watu wamekuwa wanachoma moto. Kuchoma moto siyo kosa kama utafuata utaratibu, lakini kama tunakwenda kuchoma misitu, miti iliyopandwa kwa ajili ya kutunza na kuhifadhi

mazingira, maana yake hatuwezi kwenda kwenye mashamba yetu tukalima halafu tukapanda, *otherwise* tukate matakataka halafu tuchome moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba kwa mujibu wa Sheria za Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira na kwa mujibu wa Sheria za Uhifadhi wa Misitu kule *TFS* ni marufuku kuchoma misitu kinyume na utaratibu na kutokufuata utaratibu uliowekwa, kinyume na kufanya hivyo ni kosa kisheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu kumekuwa na programu kila mwaka ya upandaji miti na kama Taifa hatujawahi kupata taarifa angalau kila mwaka ni miti mingapi imependwa na kukua ili tujue kama tumefikia matokeo chanya. Ni lini mtatoa hiyo taarifa ili kama Taifa tujue tunakwama wapi na wapi tunafanikiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, kuwa ni kweli tumekuwa tunapanda miti mingi kupitia programu tofauti za upandaji miti, lakini kupitia matukio tofauti na hasa kile kipindi kama hiki ambacho tumekimaliza juzi na tunachoendelea nacho cha Wiki ya Mazingira Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa zetu huwa tunatoa taarifa ya miti mingapi huwa tunaipanda, kwa mfano kama juzi wakati tunaelekea kuadhimisha ile Wiki ya Mazingira, tulikuwa tunatoa takwimu za miti mingapi tumepanda kitaifa, wilaya, kanda na hata mikoa na kwa sababu kwenye utekelezaji wa ilani na sheria zetu kama nilivyosema kwenye jibu la msingi,

tumeelekeza halmashauri kwa kila mwaka ipande miti isiyopungua 1,500,000.

Kwa hiyo, huwa tunatoa taarifa kila halmashauri ni mingapi, kila wilaya mingapi na kila mwaka mingapi. Sasa kama Mheshimiwa anataka taarifa tutamletea ili aone hiyo taarifa ujue tumepanda miti mingapi na tumefikia wapi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Muungano na Mazingira.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri wangu kwa majibu mazuri sana, ni *outstanding performance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile dada yangu Mheshimiwa Aida alikuwa anataka takwimu ya mwaka huu, mpaka tulivyofika mwezi Machi mwaka huu, katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa utekelezaji wa ilani ilipandwa miti milioni 266, lakini *surviving rate* ilikuwa miti milioni 211 sawasawa na utekelezaji wa 79.3%. Kwa hiyo, tunakwenda vizuri mpaka sasa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yenu kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunahamia Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa wa Tabora Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 569

**Malipo ya Pensheni kwa Wastaafu**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa wastaafu kwa wakati mafao yao?

**MWENYEKITI:** Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshasimika Mfumo wa Malipo ya Pensheni yaani *TPPS* kwa waajiri wanaolipwa mafao na Hazina pamoja na ku-*scan* majalada yote ya wastaafu na kuyahifadhi katika Mfumo wa Malipo ya Pensheni. Hii imesaidia mstaafu kupata taarifa na majibu yake kwa haraka pindi wanapotembelea Ofisi za Hazina Ndogo zilizopo katika mikoa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusiana na mafao ya hitimisho ili mstaafu ajue mfuko sahihi anaopaswa kulipiwa na aina ya mafao atakayostahili kulipwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali bado kuna matatizo mengi sana kwa wastaafu ambao wanastaafu hasa katika kufuatilia haki zao na mpaka wakati mwingine inapelekea wengi wanafuatilia mafao yao kwa muda mrefu na wengine kifo kinawakuta hawajapata hayo mafao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mfumo kuhusiana na wastaafu ili ule mfumo wa mawasiliano wa wastaafu waweze kupata fedha zao mapema? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna tabia za baadhi za waajiri kukawiza kupeleka yale makato ya wastaafu, kitu ambacho kinapelekea wale wastaafu wakati wanafuatilia wanakuta makato baadhi au mengi tu hayajafika sehemu inayohusika, je, Serikali inawachukulia hatua gani waajiri hawa ambao wanakawiza yale makato ya wastaafu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, tunaendelea na swali lako.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia sana jambo hili na jambo alilolisema Mheshimiwa Mbunge ni jambo ambalo Serikali imekuwa ikilifanyia kazi kwa ukaribu sana hasa kwa kuwaheshimu hawa wastaafu ambao walishalitumikia Taifa letu na wengine kwa rekodi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali tayari tumeweza kuweka mfumo na hiyo yote nia yake ni kupunguza hasa urasimu uliokuwa unahusisha kufanya vitu kwa njia ya kianalogia. Kwa hiyo, kwa utaratibu huo ambao tumekwishauweka tunaamini hili jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema litakwenda kwisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu waajiri ambao wanakawiza mafao, jambo hili tayari limekwishachukuliwa na Mheshimiwa Waziri anayehusika na sekta alilitolea kauli na huo ndio msimamo wa Serikali. Tutaendelea kufuatilia kwa ukaribu sana na endapo patatokea ambapo pana ucheleweshwaji wa makusudi wa aina hiyo, hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa umri mrefu ni baraka, lakini ni ahadi kutoka kwa Mungu, je, ni lini Serikali italeta sheria itakayosaidia kurekebisha pensheni wanayolipwa kila mwezi wastaafu kwa muda mrefu waendane na wenzao wanaostaafu kwa kipindi kama hiki cha sasa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeipokea hoja ya Mheshimiwa Mbunge na tutaijumuisha kwenye masuala ambayo tunaendelea kuyafanyia kazi katika kuboresha tasnia hii ya malipo kwa wastaafu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Waziri, kwa mujibu wa tafiti inaonesha kwamba *lifespan* ya wananchi kwa sasa imeshuka sana na kipindi cha kustaafu kwa hawa wastaafu wetu ni miaka 60 na kuendelea, lakini tunaona kipindi hiki ndicho kipindi chenye magonjwa mengi, maradhi mengi na ugumu wa maisha, hali ambayo inawafanya wapate *stress* sana.

Sasa je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea kile kiwango kutoka 33% ya mafao ya mkupuo kwa sasa mpaka angalau hata 80% ili wa-*enjoy* mafao yao kwa kipindi hiki chote ambacho kimebakia? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sehemu ya mwisho ya swali la Mheshimiwa Mbunge niipokee kwa sababu ni mambo ambayo tunaendelea kuyafanyia kazi na Wizara ya kisekta, lakini kipengele cha kwanza kile alichosema *lifespan* imeshuka, nadhani imeongezeka na hata sasa wanaume tunaishi sana sasa hivi. Tumesogeasogea, kwa hiyo, *lifespan* imeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kipengele cha pili ni swali la msingi aliloliuliza na ni moja ya mambo ambayo tunaendelea kuyafanyia kazi na nadhani tutaendelea kuwasiliana na Vyama vya Wafanyakazi kuhusu Serikali inasema nini juu ya suala hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, miaka ya 1985 Serikali ilistaafisha watumishi wa umma kwa mkupuo na hadi sasa wale watumishi bado wako hai.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati mwafaka wa kuangalia upya wale wastaafu waliostaafishwa kwa mkupuo ili waweze kulipwa pensheni kwa kiasi kinachowezekana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ulipaji wa mafao ni jambo lenye *formular* na inatokana na uchangiaji, lakini likiwa ni ombi mahususi tumepokea na tutaendelea kulifanyia kazi na kuangalia uwezekano kama alivyosema kwamba inatakiwa tuangalie uwezekano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kulipa mafao au madai ya wazee wetu wapiganaji wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia ambao wamebaki mpaka sasa hivi wanaendelea kudai?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo nalo lina historia ndefu, kwa wale ambao kumbukumbu zao zilisadiki kulipwa wote walishalipwa, kama kuna ambao madai yao ni *genuine* na hawajalipwa nadhani taratibu za masuala ya malipo zitafuatwa, lakini katika kumbukumbu nilizonazo wale wote ambao kumbukumbu zao zilisadiki wanastahili kulipwa walikuwa wamekwishalipwa na kama Mheshimiwa Mbunge ana maeneo mahususi au ana kumbukumbu mahususi zinazohusiana na hilo tutaonana naye ili tuweze kuzipokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Serikali itawalipa lini wananchi wa Kata ya Nyatwali ambao wanahamishwa kutoka kwenye maeneo yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa hili ni swali jipya linahusiana na fidia na hili lilikuwa linahusiana na pensheni, naomba tu nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili limekwishafika mezani kwetu na ni moja ya jambo ambalo linafanyiwa kazi kwa ukaribu. Eneo la Nyatwali, Kipunguni kule Dar es Salaam pamoja na maeneo mengine yanayohusiana na masuala ya fidia, nimepokea na tunayafanyia kazi na punde hali ya kifedha itakaporuhusu tutaendelea na ulipaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, Serikali ina mpango gani wa kulipa wafanyakazi wa Vyuo Vikuu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili na wao waweze kupata stahiki yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye moja ya swali la nyongeza, wale wote wanaodai ambao kumbukumbu zinasadiki/zinaafiki kwamba wanatakiwa walipwe, Serikali italipa, lakini kwa wale ambao kumbukumbu tulizonazo, waliowahi kufanya kazi katika maeneo hayo siku nyingi wengi wao waliokuwa wanatakiwa kulipwa walikwishalipwa.

Kwa hiyo, kama kuna wengine ambao uhakiki utaonesha wanatakiwa kulipwa, Serikali italipa kufuatana na upatikanaji wa fedha, lakini kumbukumbu tulizonazo hayo maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasemea, malipo yalikwishafanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa wastaafu na hata wasiokuwa wastaafu wamekuwa wakifuatilia sana suala la kikokotoo, je, Serikali sasa imefikia wapi ili kurekebisha habari kikokotoo kwa sababu hata ukienda kwenye majimbo yetu bado swali linakuwa kuhusu kikokotoo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa majibu kwamba katika eneo hili tulikwishakukubaliana pande zote sisi pamoja na wafanyakazi, lakini maeneo ambayo tunayoendelea kuyafanyia kazi ndani ya Serikali, tunajua maeneo ambayo tunaendelea kuyafanyia kazi, muda muafaka tutakapokuwa tumekamilisha kazi hiyo tutasema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, swali la nyongeza. Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mtwara Mjini kuna wakazi zaidi ya 600 ambao wanadai kwenye Mfuko wa *Pride* zaidi ya shilingi milioni 600. Pia Mheshimiwa Waziri uliniahidi toka mwaka 2021 kwamba mnakwenda kuwapa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri watakwenda kuwalipa wale wananchi ambao sasa hivi wanataabika na hawaelewi wapi waende ili wapate fedha zao ambazo tayari ziliingizwa kwenye Mfuko wa *Pride?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge ni kweli amekwishakuja mara kadhaa akiwa anafuatilia jambo hili kwa ajili ya wananchi wake hao 600 aliowasema kwa ajili ya madai kutoka *Pride*. Ni kweli tulimwambia kwamba tunaendelea kukamilisha baadhi ya taratibu. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge tukishamaliza maswali na majibu tukae ili mimi nikiwa na wataalamu wangu aweze kupata hatua ambayo imekwishafikiwa na Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunahamia swali linalofuata, Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi Mjini, sasa aulize swali lake na kwa niaba yake…

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sorry*…

**MWENYEKITI:** Aah, yupo yeye mwenyewe.

Na. 570

**Serikali Kudaiwa na Watoa Huduma**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE** aliuliza: -

Je, ni kiasi gani hadi sasa Serikali inadaiwa na wazabuni, wafanyabiashara, wakandarasi na walipa kodi kutokana na huduma, kazi na kodi zilizozidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa swali la Mheshimiwa Mbunge.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2024 Serikali ilikuwa inadaiwa jumla ya shilingi bilioni 1,033 ya madeni

yaliyohakikiwa ya wazabuni wa bidhaa na huduma pamoja na wakandarasi. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 1,024.26 ni madeni ya wazabuni wa bidhaa na huduma na shilingi bilioni 8.75 madeni ya wakandarasi. Hadi Machi, 2024 Serikali imeshalipa jumla ya shilingi bilioni 949.31 sawa na 92% ya madeni yaliyohakikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2024 Serikali ilikuwa inadaiwa jumla ya shilingi bilioni 80.06 ya madeni yaliyohakikiwa yanayotokana na kodi *(VAT Refunds Claims)*. Hadi Machi, 2024 Serikali imefanya marejesho ya jumla ya shilingi bilioni 675.1 sawa na 96% ya lengo kwa kipindi cha mwaka 2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, maswali ya nyongeza.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijauliza maswali yangu ya nyongeza ningetamani kiti chako kiweze kujua madeni haya ni ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, lakini pia madeni haya yanajumuisha yale madai ya wakandarasi ambayo yaliripotiwa hapa kwa upande wa Wizara ya Maji shilingi bilioni 400 na kitu, Wizara ya Miundombinu kama *TANROADS* shilingi bilioni 913 ni kwamba yanajumuisha yote? Maana yake imenishitua kidogo tu hapa kuona kwamba kuna shilingi bilioni nane tu za wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kuyasema hayo naomba niulize maswali yangu mawili ya nyongeza, swali la kwanza, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni athari gani za kiuchumi za muda mfupi, wa kati na muda mrefu ambazo Serikali na hao wazabuni na wakandarasi wanazipata kwa madai haya ya kutokulipwa kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ningetamani kusikia kauli ya Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba madeni kama haya na mengine makubwa ambayo tunayafahamu yatalipwa kwa wakati kwa kulipwa *cash* au kwenda kwenye mfumo wa kubadilisha deni kwenda kwenye dhamana ili hawa wadai walipiwe haya madeni kwenye mabenki yao na Serikali ambayo inadaiwa kuliko hawa wenye madai kuendelea kubanwa na mabenki wakati huo Serikali haijawalipa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa kuweka kumbukumbu sawa, tunaweka makundi ya madeni ama madai ya wazabuni na watoa huduma na wakandarasi wadogo wadogo katika fungu moja na kwa kuwa swali lilikuwa linauliza madai, kwa hiyo, haya yanahusisha wazabuni, watoa huduma na wakandarasi wadogo wadogo na hata malipo yake yanakuwa upande tofauti.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, mnaoendelea kushauriana naomba mpunguze sauti wakati wa mashauriano ili kumwezesha Mheshimiwa Waziri majibu yake yaweze kusikika kwa Bunge na yasikike kwa wananchi wanaotufuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia nilipokuwa nimeanzia, kwa hiyo haya ni madeni ya watoa huduma, wazabuni pamoja na wakandarasi wa *group* hili hapa, lakini hii ni tofauti na madeni ya *certificate* zile za wakandarasi wakubwa ambao wanafanya kazi kubwa zile za barabara pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu haya nadhani nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa sababu madeni haya kama mtakumbuka yalikuwa na kiwango kikubwa sana, yalikuwa zaidi ya shilingi trilioni nne kwa sababu yalikuwa hayajalipwa kwa muda mrefu sana, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani alisema fedha hizi watu walipwe ili kuweza kuchachua uchumi kwenye ngazi za Serikali za Mitaa na itakumbuka kila mwaka tukawa tunatenga zaidi ya 100% ya ongezeko la bajeti ya kulipa wazabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kuna watu wengine walishakata tamaa kuhusu kupokea fedha hizo na kuna wengine walipata shida na benki. Kwa hiyo, imeendelea kulipwa kidogo kidogo ndio maana sasa hivi ilishapungua ikafika kiwango hiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba ina madhara ama haina, ni dhahiri ina madhara mtoa huduma anapokuwa ametoa huduma na pengine amekopa, akicheleweshewa kulipwa fedha yake ina madhara na ina madhara kwenye uchumi na ndio maana Serikali imelipa yale madeni ya nyuma na imeendelea kulipa na tumetoa rai kwa Serikali za Mitaa kutokuzalisha madeni ili kuweza kuhakikisha kwamba hatukwamishi shughuli za kiuchumi na hii ni sehemu ya kuhakikisha kwamba tunaipa nguvu sekta binafsi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya benki zimeuza dhamana za baadhi ya wazabuni ambao walikuwa wakidaiwa na Serikali na wengine wamefilisika, je, Serikali inawasaidiaje wazabuni hao ambao wamefilisika kutokana na kadhia ya kuidai Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata si msaada ni haki yao, Serikali ilichofanya imejitahidi kuwalipa wazabuni wote ambao walishatoa huduma na tutaendelea kulipa bila kuzalisha madeni kwa watoa huduma ambao wameshatoa huduma, wanatoa huduma nzuri Serikalini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Serikali imekuwa ikipata hasara kubwa sana kwa kuwalipa riba wakandarasi na hii inatokana na Serikali kuchelewesha fedha za wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, je, ni kwa nini Serikali isibadili utaratibu uliopo sasa na badala yake iweke utaratibu wa kutangaza *tender* pale ambapo Serikali inakuwa ina fedha mkononi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri umepokelewa na hatua nyingine ambayo Serikali imefanya kwa mfano mikataba mingi ya miradi ya umwagiliaji hatujaweza kuweka kipengele hicho cha riba, kwa hiyo, tumepokea ushauri huo na ndio maana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alirejesha Tume ya Mipango ambayo itasaidia miradi itekelezwe ambayo iko kwenye mpango na itekelezwe ambayo ina bajeti yake ili kuepuka kuwa na miradi ambayo iko nje ya bajeti ambayo inasababisha kutengeneza riba kutokana na ucheleweshaji wa malipo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upo utaratibu mzuri Hazina walikuwa wakiutumia kuwalipa wale wanaotoa huduma kwenye shule hasa ku-*supply* vyakula, kila mwezi walikuwa wakiwalipa, lakini hivi karibuni wamekuwa wakicheleweshewa sana malipo yao na imesababisha pia washindwe kutoa huduma zao *effectively* kwenye shule zetu.

Je, mpo tayari sasa kurudisha ule utaratibu wa mwanzo wa kuwalipa kila mwezi ili huduma ziendelee kuwa nzuri na zisiathiri huduma za shule?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameelezea utaratibu wenye mafanikio, kama Serikali niseme tumepokea ushauri wa *Madam Jesca,* Mheshimiwa Mbunge wa Iringa Mjini na tutaongea na wenzetu wa TAMISEMI ili kuweza kuratibu vizuri utaratibu wa utoaji wa fedha ili shughuli za utoaji wa huduma hasa hasa kwa wanaotoa huduma kwenye taasisi zetu za Serikali uende vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na madeni ya Serikali kumekuwa na tatizo vilevile la ulipaji wa pesa za kujikimu kwa wanafunzi wa elimu ya juu *(boom)* kiasi cha kifikia kwamba wanalipwa mpaka pesa za mwisho wa mwezi huu wanalipwa mwezi ujao katikati au karibu na mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini hatua ya Serikali kuondoa tatizo hili kuwaepusha hawa wanafunzi na kuingia kwenye matatizo yasiyo ya lazima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa kwa wakati fedha za wanafunzi wa elimu ya juu almaarufu kama *boom* alivyosema Mheshimiwa Mbunge na kama kuna wakati ilitokea kucheleweshwa itakuwa wakati huo tu na hata hivi tunavyoongea tayari tulishapeleka zaidi ya shilingi bilioni 100 ndani ya kipindi hiki Bunge likiwa linaendelea na tunaamini kwamba itaenda kukidhi mahitaji yote ya wanafunzi na tulikuwa tunateta na Waziri wa sekta hapo wakati ninakuja kujibu maswali hapo kama kuna eneo lolote ambalo bado lina uhitaji Serikali itatoa fedha hizo mara moja ili watoto wetu waendelee kusoma bila tatizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako kwa Wabunge majibu ambayo ni mafupi na ya moja kwa moja inatoa fursa na kuwapa Wabunge nafasi ya kuuliza maswali mengi ya nyongeza, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea swali linalofuata ni Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Serikali tunahimiza majibu ya moja kwa moja na kwa ufupi ili kuruhusu Wabunge wengi waweze kuuliza maswali kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela aulize swali lake.

Na. 571

**Ahadi ya Kuweka Taa katika Kiwanja cha CCM – Kirumba Mwanza**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya kuweka taa katika kiwanja cha cha mpira cha CCM – Kirumba, Mwanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Ilemela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM Kirumba ni miongoni mwa viwanja vitano ambavyo vimewekwa katika mkakati wa Serikali wa kuvirekebisha ili kukidhi ubora na viwango vya *CAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara ipo katika hatua ya majadiliano na mmiliki ili kukubaliana namna ya kugharamia na kuviendesha viwanja hivyo ikiwemo uwanja wa CCM Kirumba

ambapo pamoja na marekebisho mengine, uwanja huu utawekewa taa ili kuwezesha shughuli za michezo kufanyika hata nyakati za usiku.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuwa ubora wa viwanja hauishii katika kuweka taa peke yake, je, Serikali haioni kwamba ni muhimu sasa kutengeneza hata yale maeneo ya kuchezea mpira kwa maana ya *pitch,* lakini ikiwemo pia kuboresha yale maeneo ya kukimbilia ambayo tunahitaji pia kupata akina Filbert Bayi na akina Mwinga Mwanjala wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa tunazo Halmashauri kadhaa nchini ikiwemo ile ya Manispaa ya Bukoba, Uwanja wa Kaitaba tunayo ile ya Ruangwa, Uwanja wa Majaliwa na Nyamagana pia pale katika Jiji la Mwanza, je, Serikali haioni sasa ni muhimu pia katika kushirikiana na halmashauri kuweza kupata viwanja vipya vya michezo ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela lakini pamoja na viwanja vya michezo ya ndani kama vile *netball, basketball* na michezo mingine badala ya ku-*promote football* peke yake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kama ambavyo nimejibu wakati najibu swali la Mheshimiwa Mabula la msingi, taa itakuwa ni sehemu tu ya marekebisho ambayo yatafanyika kwenye viwanja hivi tukishakubaliana na mmliki wa viwanja ambavyo tunataka kuvifanyia marekebisho, lakini kuna mengi mengine ambayo yatafanyiwa marekebisho yakiwemo majukwaa na majukwaa ya kukaa watu mashuhuri, lakini pia vyumba vya kubadilishia nguo na maeneo ya kuchezea yaani *pitch* na hata yale maeneo ya kukimbilia ili kutengeneza akina Filbert Bayi

wengine kama Mheshimiwa Mabula anavyoiweka, yatafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia namna ambavyo Uwanja wa Benjamin Mkapa unafanyiwa marekebisho yale ndiyo aina ya marekebisho tunakwenda kufanya katika viwanja hivi ambavyo tumeviorodhesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili; Serikali inafahamu umuhimu wa kuwa na miundombinu ya michezo katika majiji, manispaa na halmashauri zote nchini kwa sababu mahitaji yake hakuna sehemu ambayo hayapo na Serikali hata katika viwanja hivi ambavyo amevitolea mfano Mheshimiwa Mbunge imekuwa ikitoa ushirikiano mkubwa wa kiufundi na wataalamu wetu hasa ndio wamekuwa wakitumika kuwezesha viwanja hivi kutengezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nitoe rai sasa kwa halmashauri na manispaa zote nchini kutenga maeneo ya michezo ambayo tayari yako katika matumizi ya mpango bora wa ardhi, lakini pia kuhakikisha wanatenga fedha kugharamia utengenezaji wake na sisi kama Serikali tutaendelea kutoa ushirikiano kama ambavyo tumekuwa tukitoa katika maeneo mengine ambayo yaliweza kutengeneza viwanja hivyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa timu zetu za Yanga na Simba zimejizolea umaarifu nchi nzima na michezo yao imekuwa ikifanyika hasa kwenye miji mikubwa, lakini kuna maeneo kama wilayani ambako tayari viwanja vimeshatengwa kama Wilaya ya Nyasa ambayo ina mpango wa kujenga kiwanja cha kimataifa cha michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kuzishawishi timu hizi kubwa kucheza michezo maalumu ya kuchangisha fedha kusaidia wilaya zenye mapato kidogo kama

hizi ili wanachama wao na wapenzi wao waendelee na wao kunufaika na siku nyingine waende wakacheze na huko? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, wazo zuri la *Engineer* Stella Manyanya, lakini timu zetu zinakuwa na ratiba ambazo zimepangiwa kwa mwaka mzima na zenyewe zinajipangia ratiba zao kwa ajili ya kujiandaa kwa mashindano mbalimbali rasmi. Isipokuwa ni wazo zuri na tutalifikisha kwa timu hizi kuona kama zinaweza kufanya mpango wa kurejesha kwa jamii kwa kufanya michezo ya hisani kwenye halmashauri hizi ikiwemo Nyasa kama ambavyo Mheshimiwa *Engineer* Manyanya ameiweka hapa ili kuhakikisha wanahudumia wananchi ambao wengi ni wapenzi wa timu hizi kubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa CCM Kirumba ni sawasawa na Uwanja wa *Julius Nyerere Stadium* pale Mbulu, ulijengwa vizuri na sasa unahitaji fedha za kumalizia na Serikali mliahidi hapa Bungeni kwamba mtaweka pesa za kumalizia ule uwanja.

Je, lini mtapeleka pesa ili uwanja ule ukamaliziwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, swali zuri la Mheshimiwa Flatei Massay.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema viwanja hivi ambavyo tumepanga kuvifanyia marekebisho bado tunajadiliana na wamiliki ili kuona namna ambavyo tutaanza

kuvifanyia marekebisho na namna ya kuviendesha na uwanja wake ni moja ya viwanja ambavyo vitakuja japokuwa haviko kwenye awamu hii ya kwanza, lakini vimepangwa na vyenyewe kuangalia namna ambavyo tutavirekebisha na kuvifanyia utaratibu wa namna ya kuviendesha ili wananchi wapate miundombinu ya michezo katika jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Benjamin Mkapa ni uwanja wa umma, kwa hiyo ni sahihi kwa fedha za umma kuzitumia kuukarabati. Uwanja wa CCM Kirumba ni uwanja wa CCM, kwa hiyo, si sahihi kwa fedha za umma kutumika kukarabati uwanja wa CCM.

Swali langu kwako, ni kwa namna gani hizi fedha za umma ambazo zitatumika kukarabati uwanja wa CCM zitarudishwa ili zifanye kazi nyingine za umma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema tunachofanya sasa hivi ni majadiliano ya namna ya kuvikarabati hivi viwanja, lakini namna ya kuviendesha pia, kuviendesha kwa maana kwamba hata mapato yatakayokuwa yanatoka kwenye viwanja hivi maana yake yatakuwa yanatumika kurejesha fedha ambazo zitakuwa zimetumika kuvikarabati. *(Makofi)*

Kwa hiyo nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunachofanya ni kwenda kuhudumia umma ule ule ambao utavitumia viwanja hivi lakini pia fedha zitakazopatikana zitarudi ili kufanyia shughuli zingine za umma, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa muda wa kuuliza swali langu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe ni mkoa mchanga na ni mkoa mpya na toka tumepata mkoa tumeshatafuta tayari eneo la kujenga uwanja wa michezo eneo la makao makuu ya mkoa pale Vwawa, Mbozi. Nini mpango wa Serikali wa kusaidia tuwezeshwe kupata uwanja huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilijibu wakati najibu swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula nimetoa rai kwa mamlaka za majiji, mamlaka za manispaa na halmashauri kuona namna ambavyo wanaweza kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kutengeneza maeneo kwa ajili ya shughuli za michezo na Serikali itaendelea kutoa ushirikiano mkubwa kwenye masuala ya kiufundi na wataalamu wetu watatumika kuhakikisha hilo linawezekana kama ambavyo wamefanya katika maeneo mengine kama kule Kaitaba, Mkoani Kagera na Nyamagana, Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitalichukua jambo hili kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameliweka na kuona namna ambavyo tunaweza tukasaidiana na Mamlaka ya Mkoa wa Songwe kuona tunavyoweza kusaidia kutengeneza maeneo ya michezo hasa kiwanja hiki ambacho wameshakipatia eneo katika mkoa wao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa uwanja wa michezo Jamhuri katika Manispaa ya Morogoro kwa kiwango cha kisasa pamoja na kuweka taa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Jamhuri, Morogoro ni miongoni mwa viwanja vitano vya kwanza ambavyo

tumeviorodhesha na tunafanya mazungumzo na wamiliki ili kuanza kuvikarabati. Kwa bahati nzuri Jamhuri iko pamoja na Uwanja wa Mkwakwani – Tanga, CCM Kirumba, Jamhuri - Morogoro na Sokoine - Mbeya na tutakuwa katika awamu ya kwanza mara tutakapokubaliana na mmliki wa viwanja hivyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Jiji la Dar es Salaam ni Wilaya ya Ubungo tu ambayo haina viwanja vya michezo ilhali ina wananchi zaidi ya milioni moja na tukumbuke tayari Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alishatoa eneo la ekari 72 na ndani yake kuna ekari 11 kwa ajili ya viwanja hivi vya michezo.

Je, ni upi mkakati wa Serikali kuanza kujenga viwanja hivi ndani ya Wilaya yetu ya Ubungo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa nguvu kubwa ya Serikali hasa katika sekta ya michezo iko katika kutengeneza miundombinu ya viwanja vitakavyotumika kwa ajili ya *AFCON,* lakini tunafahamu umuhimu wa Ubungo kuwa na kiwanja chake cha michezo na nikuhakikishie tutakapomalizana na hili, hili ambalo umelileta Mheshimiwa Mbunge litakuwa miongoni mwa mambo ambayo tutayafanyia kazi kwa awali kabisa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunahamia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 572

**Utoaji wa Hati za Kumiliki Ardhi Mkoani Katavi**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Katavi wanapata hati za kumiliki ardhi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Katavi kama ilivyo kwenye mikoa mingine, Serikali inaendelea kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa wananchi kupitia Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Katavi. Hadi Mei, 2024 jumla ya viwanja 70,291 vimepangwa, 23,603 vimepimwa na hatimiliki 4,838 zimetolewa. Aidha, viwanja 12,666 vimepangwa, 8,533 vimepimwa na 698 vimemilikishwa kupitia Programu ya Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Miliki za Ardhi, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 10 imeandaliwa, vipande vya ardhi 69,216 vimetambuliwa na hati za haki miliki za kimila 23,901 zimesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi katika Mkoa wa Katavi, Serikali imeendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali ikiwemo Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK), Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Miliki za Ardhi *(LTIP)* na Miradi ya Urasimishaji wa Makazi Yasiyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa Sekretarieti ya Mkoa pamoja na Mamlaka za Upangaji katika Mkoa wa Katavi kuhakikisha kuwa wanatumia kikamilifu fursa za programu na miradi mbalimbali ya sekta ya ardhi inayotekelezwa katika Mkoa wa Katavi ili kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa

ardhi na hivyo kuimarisha usalama wa miliki za ardhi kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, maswali ya nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi vijijini wamekuwa hawajui umuhimu wa kuwa na hatimiliki na matokeo yake wawekezaji wanapofika wananchi wao wanaondolewa kwenye ardhi zao kwa kigezo cha kutokuwa na hati miliki.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa wananchi vijijini na mijini kupima maeneo yao ili kuondoa adha ya kuondolewa kwenye ardhi na mashamba yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, hati miliki za vijiji hazitambuliki kama dhamana ya kupata mkopo benki, je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa waraka kuziambia benki kuwa hatimiliki za vijiji zitumike kama dhamana ya kupata mkopo vijijini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la kwanza la Mheshimiwa Taska kuhusu utoaji wa elimu, Wizara imeendelea na inaendelea kutoa elimu kwa wananchi hasa kupitia miradi mbalimbali inayoendeshwa kwenye vijiji hivi na ifahamike kwamba wakati tunapokwenda kuanza kufanya maboresho kwenye ardhi za vijiji, cha kwanza kinachotangulia ni elimu ile ile *ownership* ya umiliki wa ule mradi uwe wa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapokwenda pale kwanza elimu kwa makundi mbalimbali ya wadau kwenye eneo lile wakiwemo wananchi wenyewe na pili, makundi saidizi ya

viongozi ambao wanasimamia masuala ya ardhi kwenye mamlaka hizi za vijiji.

Kwa hiyo, kutoa elimu tumeshaanza na tunachokwenda kufanya ni kutoa elimu ya jumla ambayo itahusu maeneo yote ambayo yamepitiwa na mradi au hayajapitiwa na mradi ili watu wajue taratibu za jinsi ya kuthamini ile hati wanayoipata kutokana na mazingira ya uwekezaji inapojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni hatimiliki na thamani yake kwenye vyombo vya fedha, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote, zile hatimiliki kwa sasa zinatumika. Benki zilishapewa mwelekeo wa kutambua thamani ya zile hati na mpaka sasa tuna ushahidi wa kutosha wananchi wanakopa fedha kwenye benki zetu kupitia zile hatimiliki za kimila.

Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi wananchi, waende kwenye benki hizo na pale patakapotokea changamoto tuwasiliane na Wizara ili tuweze kuwasaidia zaidi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, je, ni lini Serikali itaweka mpango wa matumizi bora ya ardhi pamoja na kutoa hatimiliki kwa wananchi wa vijiji vya Mshara, Uduru, Lyamungo, Mnadani, *Sanya Station,* Mtakuja, Chemka, Rundugai, Isiki na maeneo mengine yote ya Jimbo la Hai ambao hawajapata hatimiliki?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Saashisha amekuwa na juhudi kubwa ya kufuatilia wananchi wake maeneo yao kupimwa. Mheshimiwa nataka tu nimwahidi katika mpango unaondelea tutaingalia Hai katika jicho

la pili kwa maana ya kuiweka kwenye mpango ili wananchi wale waweze kunufaika na miradi hii ya maboresho ya ardhi katika maeneo yao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kama jitihada za kuwandaa wananchi wa Ludewa kwa miradi ya Mchuchuma na Liganga imeingiza vijiji vyote kwenye Mradi wa Mipango ya Matumizi Mora na kutoa hatimiliki za kimila. Vilevile ilitoa shilingi milioni 400 kwa ajili ya urasimishaji ambapo viwanja 14,000 vimeshapimwa, lakini wilaya hii ina watumishi wanne tu.

Je, ni lini Serikali itawapeleka watumishi ili waweze kwenda kutoa hatimiliki na kusimamia mipango hii mizuri ya Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekuwa na upungufu mkubwa wa watumishi katika maeneo mbalimbali hapa nchini na sasa tunaendelea na zoezi kutokana tu na mgao tunaoupata wa namba ya watumishi ambao Wizara inapewa kuajiri kwa mwaka. Nikutoe tu wasiwasi kwamba hivi karibuni kwenye ajira zinazokuja tutaiangalia Ludewa kama sehemu maalumu ya kuongeza nguvu ya watumishi kwenye eneo hili, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wengi wanapoenda katika halmashauri zetu kuomba huduma ya kupimiwa ardhi kumekuwa na sababu nyingi ambazo zinawafanya wasipimiwe ardhi kwa wakati, mfano ukosefu wa vifaa, rasilimali watu na mambo mengine, jambo ambalo linachangia utoaji wa rushwa ili mwananchi apate huma hiyo.

Nini kauli ya Serikali kuweka utaratibu uliobora ambao unaeleweka kwa wananchi ili wananchi waweze kupata huduma hii?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Paresso rushwa ni ugonjwa kama ugonjwa mwingine wa malaria, yaani haisimamiwi kwa sababu ya ukosefu wa vitendeakazi na hili ni tatizo na tunaendelea kupambana nalo. Niwaombe wananchi wote, pale ambapo mtumishi wa mamlaka hii anapoomba rushwa, naomba sana mtoe taarifa kwenye vyombo ambavyo vinahusika na masuala haya ya usimamizi wa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu suala la utaratibu wa kutambuliwa maeneo yao na kupimiwa, nimtoe wasiwasi tu, katika programu tunazokwenda nazo tuna Mradi wa KKK unasimamiwa na halmashauri karibu zote nchini na tuna huu Mradi wa *LTIP* unaolenga kuimarisha *the same* kama ilivyo kwa halmashauri. Tunachoweza kukuahidi ni kwamba programu zinazoendelea zinakwenda kuhakikisha kwamba jambo hili linaenda kwa uharaka na kuhakikisha kwamba miji yote inapimwa na kuwekwa katika matumizi yaliyo sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, unajibu swali moja tu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, eneo langu la Mgodi wa *Barrick North Mara* ambao unachukua kata tano na vijiji 11, changamoto kubwa iliyopo ni kwamba ardhi ile haijapimwa na wananchi wangu hawana hatimiliki, kwa hiyo, kulipwa fidia wanakadiriwa.

Ni lini Wizara ya ardhi itahakikisha kwamba wananchi wanapata hatimiliki ili walipwe fidia ya maeneo yao kwa mujibu wa sheria na kwa kiwango cha bei ya soko? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali zuri la Mheshimiwa Mwita Waitara, ninamwahidi tu kwamba baada ya hapa tutaonana ili tuangalie mwelekeo wa namna tutakavyolikabili hili eneo la Barrick ili wananchi waweze kutendewa haki inayostahili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Condester, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa migogoro kadhaa ya ardhi ndani ya Jimbo la Momba na kuibuka kwa mfumo wa ukabaila yaani watu kujimilikisha ardhi kinguvu, ni upi mpango wa Serikali kuja kutusaidia, Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na halmashauri kuhakiki hati zote za ardhi ambazo ziko ndani ya Jimbo la Momba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hata Waziri wangu jana alikuwa maeneo hayo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba huduma

hii inatolewa, lakini sisi hatuna ukabaila, tulishauondoa siku nyingi sana na ninaomba kwenye vichwa vya Waheshimiwa Wabunge tusiweke ukabaila kwa sababu ardhi ya Tanzania katika kupatikana kwake kuna aina mbili tu, kuna ile ardhi ya jumla ambayo wasiamamizi ni Wizara ya Ardhi na kuna ardhi za vijiji ambazo wasimamizi wake ni Serikali za Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba kwenye Serikali za Vijiji kumekuwa na changamoto nyingi, Wenyeviti wanajiuzia maeneo tu kiholela na hii niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge tuwe na sauti moja katika kuhakikisha kwamba tunasimamia na kuwasaidia wale viongozi wa vijiji katika uhalisia. Kwanza, hawastahili kuuza kipande cha ardhi kinachozidi ekari 50 lakini unakuta kwenye maeneo haya wanauza tu kiholela holela bila kujali mazingira hayo na kama kuna matukio haya naomba yaripotiwe ili twende kuyarekebisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, changamoto kubwa katika suala la hati za kimila kwa wananchi wetu ni kushindwa kukopesheka katika taasisi za fedha licha ya kwamba Serikali inasema wanakopesheka, lakini ni kwa ndogo sana na tatizo lililopo ni Sheria Namba 5 ya mwaka 1999 ambayo imezipa mamlaka Serikali za Vijiji, zinaweza zikauza ardhi ile na benki zimekuwa zikisuasua kutumia hati hizo.

Swali langu sasa je, ni lini Serikali italeta marekebisho ya sheria ili Serikali za Vijiji zisiwe na mamlaka juu ya ardhi katika maeneo hayo na wananchi waweze kukopesheka katika maeneo ya vijiji? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea wazo la Mheshimiwa Atupele na kwamba kutokana na uhalisia tunakwenda kufanya mabadiliko mbalimbali kupitia sheria zetu

kwa sababu tayari tumekamilisha Sera ya Wizara ambayo katika mazingira yale lazima sheria zifanyiwe mabadiliko. Tunakwenda kuangalia tofauti zinazotajwa na Mheshimiwa Mbunge kwamba zinaweza zikawa chanzo cha wananchi kutokopesheka, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunahamia Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 573

**Kujenga kwa Kiwango cha Lami Barabara Zinazounganisha Reli ya *SGR***

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa ujenzi wa vipande vya barabara za lami kuunganisha barabara kuu na reli ya *SGR* ili kurahisisha wasafiri kufika stesheni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko katika hatua mbalimbali za kujenga kwa kiwango cha lami barabara zote zinazounganisha stesheni za reli ya *SGR*. Kwa sasa tumeanza na stesheni zote za kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ambapo ujenzi wa reli ya *SGR* uko katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mkoa wa Pwani, taratibu za manunuzi ya ujenzi wa barabara ya Mlandizi hadi *Ruvu Station (SGR,* kilometa 22) ziko katika hatua za mwisho, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza na naishukuru Serikali kwa majibu mazuri ambayo imenipatia juu ya kipande hiki walichokizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, pamoja na kupanga kipande cha kutoka Mlandizi kwenda Ruvu na kiko katika hatua ya mwisho ya manunuzi, lakini barabara hiyo ambayo inatokea Mlandizi kwenda Ruvu ni moja ya barabara ya kutokea Makofia – Mlandizi – Mzenga hadi Vikumburu. Sasa wakati tunaendelea kutaka kwenda hatua ya mwisho ya manunuzi, Serikali imefikia hatua gani juu ya fidia ya watu ambao wako kwenye barabara hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa majibu ya Serikali yanaonesha kwamba tuko kwenye hatua ya mwisho ya manunuzi, sasa ningependa kujua ni lini mkandarasi ataingia *site* na kuanza kazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza yote kwa pamoja ya Mheshimiwa Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi barabara zote zinazokwenda kwenye *station* za *SGR* ni suala ambalo lilitakiwa lifanyike haraka sana kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ili tusije tukawakwaza ama tukawakwamisha wananchi ambao wanatakiwa watoke kwenye barabara kwenda kwenye vituo vya *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba tutakachofanya hapa kwa sababu barabara hii ilikuwa haijasanifiwa, mpango uliopo ni sanifu jenga. Kwa hiyo, watasanifu na kuendelea na ujenzi kuliko

tungetumia ule utaratibu wa kawaida wa kusanifu, halafu uje ujenge; hiyo itaharakisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusu fidia, bahati nzuri ni kwamba hii barabara kilometa 22 kuna sehemu kubwa ambalo ni eneo la Serikali, lakini ile sehemu ambayo ni ya wananchi wakati wanasanifu yale maeneo yote ambayo yatapitiwa na barabara tutahakikisha kwamba tunajenga kwa sababu ni suala ambalo ni la haraka ili tusije tukakwambisha.

Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi wa Kibaha kwamba wakati tutakapoona barabara itakapopita basi wananchi hao watalipwa hiyo fidia ili kupisha ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza ujenzi wa barabara kilometa 25 kwa kiwango cha lami katika maingilio ya Daraja la Sibiti kwa kuwa Serikali tayari ilishamkabidhi mkandarasi *site*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kilometa 25 ambazo ni maingilio tulishamkabidhi mkandarasi na namhakikihia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari mkandarasi huyo ameshaelekezwa aanze kazi haraka iwezekanavyo na hasa baada ya mvua kukatika kwamba aanze kujenga hizo kilometa 25 ambazo kwa kweli baada ya mvua pamekuwa na changamoto kubwa sana kwani barabara ilikuwa imeharibika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Barabara ya Holili mpaka Tarakea katika Wilaya ya Rombo itawekwa lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, hii Barabara ya Holili Tarakea wenzao wanaiita *Lower* Moshi, tayari ishakamishwa usanifu wa kina; bahati nzuri nimeitembelea na hata Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi amaitembelea na tuko kwenye mpango wa kuianza hiyo barabara kwanza kwa kuanza na kilometa 10.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge na Mbunge wa jimbo kwamba tayari tumeshaiingiza kwenye mpango na tunaanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Rais Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete iliyotolewa miaka 14 iliyopita ya kufungua na kujenga barabara kutoka Kipatimu kupitia Nandete kwenda Nyamwage? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hiyo ilikuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia. Nadhani Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba hatua ambazo tunakwenda kuzifanya sasa ni kwenda kuifungua hiyo barabara kama ahadi ya Rais ilivyokuwa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kutoka Mkuzi mpaka Mlola kuna kilometa 34 na

Serikali iliahidi kwamba itajenga kwa kiwango cha lami. Je, ni lini kazi hiyo itaanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia vizuri Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, naomba urejee swali lako tafadhali.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kutoka Magamba - Mkuzi hadi Mlola ni kilometa 34 ambapo ndiyo lami ilipoishia. Serikali iliahidi kwamba itajenga kilometa 34 kwa kiwango cha lami. Je, ni lini kazi hiyo itaanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali iliahidi na tulishaanza, hii barabara tunategemea tuijenge yote lakini kwa sasa tunaendelea kujenga kwa awamu na tutaendelea kufanya hivyo wakati tunatafuta fedha ili kuijenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi ambako vivuko vya *SGR* vinapishana na barabara vimeshajengwa tayari, lakini sehemu nyingi havijawekwa lami juu na hivyo kumekuwa na adha kubwa sana kwa wananchi wanaoishi karibu na vivuko hivyo. Ni lini vivuko hivyo vitakamilishwa ili tuweze kupita kwa urahisi?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jonas Zeeland.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali la nyongeza, mwaka 2022 Serikali iliniahidi baada ya kuuliza swali hapa kwamba…

**MWENYEKITI:** Samahani kidogo Mheshimiwa Jonas, naomba uketi tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali la Mheshimiwa Francis Mtinga.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba vivuko vyote ambapo barabara zinakutana na *SGR* zimeshajengwa ama madaraja yameshajengwa na tumeshawasiliana na wenzetu wa Uchukuzi kuhakikisha kwamba wakandarasi wale ambao wamejenga barabara pale Bahi na hapa Mkonze kuhakikisha wanarudisha kwenye hali ya kawaida na hasa kuweka lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tulishaiona na muda siyo mrefu watarudishia lami ili kufanya maeneo yale yasiwe hatarishi kwa watumiaji wa barabara, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jonas Zeeland, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwaka 2022 niliuliza swali Bungeni, lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami kutoka Turiani – Mziha? Mkanijibu, mtaanza katika mwaka wa fedha 2022/2023, ukapita, hola, hakuna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023 niliuliza tena swali hilo hilo mkanijibu mtaanza ujenzi mara moja kwa kuwa mmeshatenga kwenye bajeti, ikapita, hola. Mwaka 2024 nauliza kwa mara nyingine hapa, lini mtaanza ujenzi wa lami kutoka Turiani kwenda Mziha kuelekea Handeni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha na hata kama Mheshimiwa Mbunge ataona bajeti yetu, tumetenga kuendelea na ujenzi wa barabara

hiyo kilometa 30 na ndiyo zimetengwa kuanza mwaka huu wa fedha ambao tunauendea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 574

**_TANAPA_ Kumaliza Jengo la Upasuaji Kituo cha Afya Hunyari – Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, lini *TANAPA* itamalizia jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Hunyari – Bunda?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri Mheshimiwa Kitandula, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *TANAPA* imeweka utaratibu wa kufadhili miradi ya ujirani mwema kwa maeneo yanayozunguka Hifadhi za Taifa. Kupitia utaratibu huu, kati ya mwaka 2020/2021 na mwaka 2022/2023 *TANAPA* ilitumia jumla ya shilingi 144,268,404 kujenga nyumba moja ya mganga na vilevile kujenga nyumba ya *nurse* pamoja na kutengeneza samani kwa ajili ya Kituo cha Afya Hunyari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendelea kunufaika na miradi ya ujirani mwema ambayo ni sehemu ya manufaa ya shughuli za uhifadhi na utalii, Serikali kupitia *TANAPA* inatoa rai kwa wananchi wa Kijiji cha Hunyari, Wilayani Bunda, kutumia utaratibu uliowekwa katika kufadhili miradi ya ujirani mwema kwa kutuma maombi rasmi kuhusiana na umaliziaji wa jengo la upasuaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru *TANAPA* kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendeleza ujirani mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka 2020/2021 na 2021/2022 *TANAPA* iliahidi kujenga jengo la upasuaji katika Kituo cha Afya Hunyari na bahati nzuri jengo hilo limejengwa yamebaki madirisha, milango na vitu vingine vya kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuwa Serikali imeshajenga kituo cha afya pale jengo la upasuaji ndiyo limebaki na vifaa vyote vya upasuaji vimeshafika vimetunzwa kwenye vyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara ya Maliasili kwa kupitia *TANAPA* wanaweza kutafuta fedha za dharura kumalizia lile jengo la upasuaji ambalo wamelijenga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, *TAWA* waliahidi kujenga jengo la kujifungulia katika Zahanati ya Maliwanda na kwa sababu eneo la kujifungulia lina chumba kimoja na watu wameongezeka sana, akina mama wakienda pale wanashindwa kujifungua wengine wanajifungulia nje.

Je, ni lini *TAWA* itatimiza ahadi yake ya kujenga chumba cha kujifungulia cha watoto Maliwanda ambapo vifaa vyote na vifaa tiba vyote vimeshawekwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge maswali yake mawili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa miradi hii ya ujirani mwema ni kuwawezesha wananchi kuona faida ya wao kuwa karibu na hizi hifadhi. Sisi tutakapopata maombi rasmi tutaweza

kwenda kufanya hiki ambacho amekiomba Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba wananchi wa kijiji kile watumie utaratibu huu na bahati nzuri wanaufahamu, watumie utaratibu rasmi wa kuleta maombi ili tuweze kwenda kumalizia jengo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la *TAWA*, namwomba Mheshimiwa Mbunge tukutane baada ya kikao hiki ili aweze kunipa *details* za jambo hili na niweze kufuatilia kwa ukaribu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu kwenye mjadala wa Wizara hii, niliomba kwamba Serikali ifikirie namna gani itatoa rambirambi au *some sort of* fidia kwa yule kijana ambaye aliacha familia baada ya kupigwa risasi na wahifadhi. Je, Serikali imeshawaza hilo jambo au mnasemaje? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake moja la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshatoa maelekezo na watu wetu wa *TAWA* wanalishughulikia jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi, je, ni lini *TANAPA* watafikiria kutuwekea lango la kuingilia watalii kwenye Hifadhi ya Mwalimu Nyerere kwa Wilaya ya Liwale ukizingatia eneo kubwa la Hifadhi ya Mwalimu Nyerere iko Liwale? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu swali lake Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapitisha bajeti yetu hapa na tunawashukuru sana kwa kutupitishia bajeti ile, tulionesha maeneo ya kipaumbele ambayo tunaanza nayo. Naomba ndugu yangu Mheshimiwa Kuchauka awe na subira, kwa jinsi ya upatikanaji wa fedha tutaenda kufanya jambo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Tunahamia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Simon Songe aulize swali.

Na. 575

**Vyama vya Ushirika Kutumika Kuuza Nyavu za Uvuvi**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE K.n.y. MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatumia Vyama vya Ushirika kuuza nyavu za kuvua samaki zenye viwango?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mujibu wa Sera ya Uvuvi ya mwaka 2015, Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 na marekebisho yake yote inalo jukumu la kusimamia, kulinda na

kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini ili ziwe endelevu kwa kizazi hiki na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Sera ya Uvuvi inahamasisha sekta binafsi, jamii, mashirika yasiyo ya Kiserikali na vyama vya ushirika vyenye kujihusisha na masuala ya uvuvi kushiriki katika kusimamia, kutumia na kuendeleza rasilimali za uvuvi nchini kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) imetoa utaratibu wa kuingiza na kuuza nyavu za uvuvi nchini ambapo kila anayekidhi vigezo vilivyowekwa kitaalamu vikiwemo Vyama vya Ushirika vinaruhusiwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za uvuvi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Simon Songe.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni, Serikali imetoa zuio la matumizi ya nyavu za dagaa zenye meta 80 mpaka meta 120 na kusema watengeneze nyavu ambazo hazitazidi meta 60 na kina cha meta 20. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza muda kwa sababu muda uliotolewa ni mpaka tarehe 15 Juni, 2024 ambayo ni Jumamosi wiki hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka *commitment* ya Serikali, haioni haja ya kuongeza muda kwa wavuvi ili kufanya maandalizi ya kutosha kwa sababu zoezi hili linahitaji mafunzo pamoja na mtaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa nini Serikali haijafanya utafiti kuwafahamu wanaoingiza nyavu haramu hasa za makokoro ili kuwachukulia hatua za haraka na kuacha kuwafilisi wavuvi wetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la zuio la nyavu. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia wavuvi wake katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili zuio la nyavu na hili niliseme hapa hadharani kwamba zuio hili ni zuio la kitaalamu. Tumegundua kwamba zile nyavu ambazo wavuvi wetu wamekuwa wakizitumia zimekuwa zikichukua mpaka mazalia ya dagaa wadogo wadogo ambao bado hawajafikia umri wa kuvuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumekuja na maelekezo hayo kwamba sasa tunatoka kwenye matumizi ya nyavu hizo tutakwenda kwenye matumizi kadiri ambavyo wataalamu wetu wameelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muda, Mheshimiwa Mbunge tumelichukua, nimuagize Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Shemdoe, kulifanyia kazi kwa kuzingatia maelekezo hayo na kama mwisho ni tarehe 15 Juni basi aone namna ya kuongeza kidogo ili wavuvi wetu waweze kujiandaa na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili kuhusiana na makokoro, nililisema wiki iliyopita kwamba makokoro ni changamoto na mengi yamekuwa yakitengenezwa na wavuvi wenyewe tena pembezoni mwa ziwa kwa kujificha, lakini Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kwa kufuatilia kujua ni wapi yanapotengenezwa, lakini mpaka sasa hakuna kiwanda maalumu ambacho kinatengeneza makokoro kwa sababu makokoro yapo kinyume cha sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wavuvi popote pale walipo wanafahamu kwamba makokoro hayaruhusiwi kwa mujibu wa sheria na popote pale ambapo kuna mtu ana taarifa za ziada juu ya utengenezaji wa makokoro mahali popote ndani ya nchi yetu tuko tayari kuchukua hatua za kisheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Aleksia.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu wa upatikanaji wa samaki katika mito na maziwa yetu hapa nchini ambao unatokana na uvuvi haramu kwa kutumia makokoro au nyavu zenye matundu madogo madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango au mkakati gani wa kuelimisha wavuvi hao ili wafahamu na waache kutumia hizo nyavu na hatimaye kukomesha kabisa na tuweze kupata samaki ambao watakuwa kwa viwango kuliko sasa hivi ambapo hawafahamu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumeendelea kutoa elimu kwa wavuvi kwa maeneo mbalimbali, maeneo ya mito, maziwa na mabwawa. Tunaendelea kutoa elimu kupitia Maafisa Uvuvi wetu walioko katika halmashauri zetu na Wizarani na tuko tayari kuendelea kutoa elimu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu siyo kwamba hawajui madhara ya makokoro, wanafahamu, isipokuwa kinachofanyika hapa ni kama uhalifu mwingine tu ambao unaweza ukafanywa na mhalifu yeyote aliyeko katika sekta hiyo. Kwa hiyo, hawa wanaoendelea kutumia makokoro na nyenzo nyingine za uvuvi ambazo haziruhusiwi kisheria ni uvunjifu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafahamu sheria zipo, wanafahamu vinavyotakiwa kutumika ni vipi, lakini wanafanya makusudi kwa ajili ya kuvunja sheria na kujipatia kipato ambacho siyo halali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ziwa Tanganyika, Kata za Kizumbi, Wampembe na kata nyingine zinazozunguka ziwa kumekuwa na nyavu haramu ambazo zinaitwa filimayaa. Filimayaa zimekuwa na sumaku ambayo ina uwezo wa kuvuta samaki hata akiwa kilometa 100. Je, Serikali ina mpango gani wa kukomesha nyavu hizi haramu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwa na hizi nyenzo kinyume cha sheria zinazoitwa filimayaa na tumeshatoa maelekezo katika mamlaka zote za Serikali zinazohusika katika maeneo yote yanayozunguka Ziwa Tanganyika na maeneo mengine kwamba filimayaa ni marufuku na wavuvi wote hawaruhusiwi kutumia nyenzo hii kwa sababu iko kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu wanafahamu kwamba Serikali imeshatoa katazo la matumizi ya filimayaa. Wakati mwingine nyenzo hizi zinaingia kinyume cha sheria ndani ya nchi yetu na wakati mwingine kwa sababu sisi tuna lango kuu la kutoka bandarini kwenda nchi za jirani, wavuvi wengi wamekuwa wakitumia mbinu ya kuzifanya kama nyavu hizi ziko *on transit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyavu inapokuwa inakwenda kwenye nchi jirani kama Zambia na maeneo mengine ambako zinakubalika kwa matumizi zimekuwa zikiwa kama zinapita kwenda kwenye nchi hizo, lakini kwa njia ya uchepushaji zinajikuta zimerudi nchini kwa njia za giza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaendelea kufuatilia na tutaendelea kutoa msisitizo kwa mamlaka zote za Serikali zilizoko huko chini kuhakikisha kwamba zinachukua hatua kali kwa wavuvi

wote wasiozingatia sheria na wanaotumia nyenzo ambazo haziruhusiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, tuendelee kushirikiana katika hili ili tuweze kukomesha uvuvi haramu katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunahamia swali linalofuata, Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 576

**Chanjo kwa Wanyama**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa Serikali kuhakikisha wanyama wanapata chanjo ili kudhibiti magonjwa ya wanyama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha mifugo inachanjwa kwa wakati ili kudhibiti magonjwa ya mifugo ikiwemo kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuchanja mifugo kupitia vyombo vya habari, maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya Nanenane, Sabasaba na programu mbalimballi za utoaji elimu kwa umma na mafunzo rejea kwa wataalamu wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mwingine unaotekelezwa na Wizara unahusu uchanjaji wa lazima wa mifugo ambapo mwaka 2020 Wizara iliandaa Kanuni za Chanjo na Utoaji wa Chanjo yaani *The Animal Disease Vaccine and Vaccination Regulations* za mwaka 2020 ambazo zinamtaka mfugaji kuchanja mifugo yake kuendana na kalenda ya uchanjaji wa magonjwa ya mifugo. Aidha, kupitia mkakati huo, Wizara imeainisha magonjwa

13 ya kipaumbele ambayo yanadhibitiwa kwa kutumia chanjo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kusuasua katika kutekeleza sera hii ya uchanjaji wa lazima, nini mkakati wa Serikali kuendelea kutoa elimu na kuhakikisha sera hii inazingatiwa kwa uhakika zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nini mpango wa Serikali kutoa elimu kwa wafugaji kwa sababu wengi wamekuwa wakitumia *antibiotic* kiholela ambazo baadaye zinaleta athari kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikataka kujua Serikali imepanga nini kutoa elimu kwa watu hawa ili waweze kuzingatia jambo hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la kutoa elimu kwa wafugaji kutokutumia *antibiotic* kiholela. Ni wazi kwamba mifugo yetu hii hasa ng'ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika wanaishi kama ambavyo binadamu wanatakiwa kuishi, wanaumwa na baadaye wakizidiwa wakishindwa kutibiwa basi wanakufa. Kwa hiyo, natoa rai kwa wafugaji wote kwamba mifugo yetu hii lazima tuichanje ili iwe na ubora kwa matumizi ndani ya nchi na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili wafugaji wetu ni lazima wajue kwamba mifugo hii inapokuwa inaumwa, ni vizuri kuwasiliana na Maafisa Mifugo wetu ili waweze kufika kwenye eneo husiku, waangalie mfugo huu unaumwa nini ili waweze kushauri ni aina gani ya dawa inatakiwa kutumika, siyo tu kuchanja, kuwapa dawa na kuwalisha dawa ambazo haziendani

na ugonjwa wanaoumwa, mwisho wa siku tunaweza tukapelekea mfugo huo kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo natoa rai kwa wafugaji wote, mfugo unapokuwa umeumwa, ni vizuri kufanya mawasiliano na Maafisa Mifugo ili waje waone, waweze kutoa ushauri ni aina gani ya ugonjwa, kwanza wampime ng'ombe huyo, kama ni mbuzi wampime na wajiridhishe ni ugonjwa gani anaumwa, kisha waweze kumtibu kadiri ambavyo inatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili la chanjo, uchanjaji ni kweli limekuwa ni zoezi la kusuasua na ndiyo maana tulivyoona zoezi hili limekuwa la kusuasua, hii ni kwa sababu mfugaji anaona ni gharama kuingia kuchanja ng'ombe wake, lakini haoni baada ya kuchanja huko kuna faida kubwa sana kwenye mifugo yake. Serikali imekuja na mpango madhubuti na tunashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, hivi juzi mlitupitishia bajeti, mwaka huu kuanzia mwezi Julai, tutapitisha chanjo ya lazima kwa wafugaji wote na jumla ya shilingi bilioni 29 imetengwa kwa kazi hii maalumu na wafugaji wote wanapaswa kuonesha ngo'ombe wao wako wapi, mifugo yao iko wapi, mbuzi wako wapi, kwa ajili ya kupata chanjo na chanjo hii itasaidia sana kuboresha mifugo yetu ndani ya nchi ili waweze kupata soko nje na ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mwaka huu tutakuja na chanjo hiyo na itakuwa ni ya lazima kwa wafugaji wote. Wafugaji wote lazima walete ng'ombe wao, mifugo yao yote ili iweze kupata chanjo hiyo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mariam Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Maafisa Mifugo wengi wamekuwa hawawafikii wafugaji vijijini, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Maafisa Mifugo hawa wanawafikia wafugaji vijijini ili waweze kupata huduma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hiyo *concern* ya Waheshimiwa Wabunge wengi kwamba maafisa ugani hawafiki kwa wafugaji. Nasema tu kwamba ni kweli Wizara imelichukua jambo hili na inalifuatilia kwa karibu sana ikiwa ni pamoja na kutoa semina kuwapa maelekezo Maafisa Ugani hawa ili waweze kufika kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi maafisa ugani hao walichokuwa wanalalamika hasa ni kwamba usafiri wa kuwafikisha kwa wafugaji, inakuwa ni changamoto. Wizara imeshagawa zaidi ya pikipiki 120 kwa ajili ya maafisa ugani wote nchini na tunaendelea kugawa kadiri ya upatikanaji wa bajeti unavyowezekana, lakini lengo la Wizara ni kuhakikisha kwamba maafisa ugani wanafika kwa wafugaji wetu na kutoa elimu stahiki ikiwa ni pamoja na kufuatilia mwenendo wa mifugo yetu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha zaidi kabisa, natoa rai sana kwa maafisa ugani, maeneo mengi katika nchi yetu wamejigeuza kuwa ni Maafisa Masuuli wa Halmashauri. Wanakwenda kukusanya mapato, kazi wanayoifanya sasa ni kukusanya mapato tu kwenye halmashauri zetu, wanasahau kazi ya msingi ambayo imewapeleka kwenye vijiji hivyo ni kwa ajili ya kusaidia wafugaji, kwa ajili ya kusaidia mifugo inayopatika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natoa rai kwamba kila afisa ugani na kila afisa mifugo katika Taifa hili, afanye kazi aliyosomea, afanye kazi iliyompeleka kule kijijini kwa faida ya wafugaji wetu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 700 na zaidi kwa ajili ya kuhakikisha inakarabati mnada wa mifugo pale Mhunze, lakini changamoto kubwa imejitokeza ya kuwepo na chemchem katika eneo lile la mnada wa upili wa siku zote.

Je, Serikali iko tayari kuungana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Ofisi ya Mkurugenzi kuhakikisha kwamba fedha zile zinaelekezwa katika eneo jipya lililotengwa ili fedha zile zikajenge mnada ule na mnada ule ukawe na tija na ile *value for money* ikaonekane baada ya fedha zile kuwa zimetumika?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kishapu kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia jambo hili. Sisi Wizarani tumeshalichukua jambo hili na ushauri wetu ni kwamba kama eneo linaonekana halina sifa na halmashauri imeshatenga eneo lingine na tayari lina hati na mko tayari kwa matumizi ya soko, Wizara hatuna pingamizi na jambo hili namwelekeza Katibu Mkuu - Wizara ya Mifugo na Uvuvi, alifanyie kazi jambo hili na fedha hizo zielekezwe kwenye eneo ambalo wao walioko huko wameshauri soko lijengwe wapi kwa sababu wao ndiyo wanaishi huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizarani hatuwezi kulazimisha soko tukajenge wapi ambapo ninyi halmashauri mnasema hapafai. Sisi tunataka mawazo yenu ninyi mnaposema panafaa, basi sisi tupo tayari kujenga soko hilo kwa mujibu wa utaratibu uliopo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunahamia Wizara ya Afya. Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake na swali lake linaulizwa kwa niaba, karibu Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

Na. 577

**Vifaa Jengo Jipya la Mama na Mtoto Hospitali ya Meta – Mkoani Mbeya**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI K.n.y. MHE SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa kwenye Jengo Jipya la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Meta, Mkoani Mbeya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu.

**WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 5.4 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya jengo la huduma za mama na mtoto katika Hospitali ya Kanda Mbeya ambapo manunuzi ya vifaa na vifaa tiba hivi tayari vimeshafungwa na ufungaji umekamilika na jengo linatumika kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi kwa akina mama na watoto wachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na upatikanaji wa hivi vifaa tiba katika hospitali hii ya kanda, tunaishukuru Serikali ni hatua nzuri, lakini wagonjwa wanaougua saratani wana changamoto kwamba hulazimika kwenda Hospitali ya *Ocean*

*Road* – Dar es Salaam ama hapa Benjamin Mkapa – Dodoma kwenda kupata hizo huduma.

Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia wagonjwa hawa wasipate usumbufu kwa kuwajengea kitengo na kuwawekea vifaa tiba vya kutibu saratani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Ummy kwa sababu alinisaidia kule kwenye jimbo langu kunipatia vifaa tiba katika Vituo vya Afya vya Umbwe na Uru Kihaseni.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutusaidia vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Uru Kusini ambacho ni kipya kimejengwa na Serikali na karibu kinaanza kazi? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kwa maswali yake mazuri, swali la kwanza kuhusu upatikanaji wa huduma za matibabu ya saratani katika Mkoa wa Mbeya na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, ni jambo kwa kweli ambalo na sisi tumeliona kama Serikali na tayari katika bajeti ambayo Bunge letu mmetupitishia, tumeweka fedha ya kuanza ujenzi wa kituo cha matibabu ya saratani kwa ajili ya wakazi wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaamini ujenzi wa kituo hiki hautanufaisha Mkoa wa Mbeya, lakini pia watu wa Katavi, Rukwa, Njombe na Iringa. Kwa hiyo, tunaamini hawatapata changamoto ya kusafiri umbali mrefu kwenda *Ocean Road* au kuja Dodoma kwa ajili ya matibabu ya saratani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu upatikanaji wa vifaa tiba kwa ajili ya Kituo cha Afya Uru Kusini, tuseme pia kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Afya, tumetenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba na tutavisambaza katika vituo vyote vya afya na hii ni kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameifanya katika nchi yetu kuhakikisha vifaa

tiba vya kisasa vinapatikana katika ngazi ya zahanati na ngazi ya vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, mimi naamini kabisa wananchi wako watapata vifaa tiba kabla ya Uchaguzi Mkuu, mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itapeleka vitanda maalumu vya kujifungulia katika Hospitali za Wilaya zilizopo Mkoa wa Lindi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najibu swali la Mheshimiwa Maimuna Pathan, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha huu ambao tunaumaliza kesho kutwa, tumesambaza vitanda vya kujifungulia katika majimbo yote, siyo hospitali za wilaya, majimbo yote 214 ya Tanzania Bara.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuendelea kuwasisitiza *MSD*, nilitoa maelekezo, vitanda hivi vikakabidhiwe kwa Waheshimiwa Wabunge ili wao waweze kuvipeleka katika hospitali mbalimbali na vituo vya afya mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao watakuwa hawajavipata, tutaendelea kutoa orodha, lakini tayari tumeshatenga fedha ya kusambaza vitanda katika hospitali zote za majimbo yote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Labda Mheshimiwa Waziri, urejee tena hayo maelekezo yako kwa sababu kwa sehemu hayazingatiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, siyo kwa miradi hiyo tu, yapo baadhi ya magari yalielekezwa yakabidhiwe na Wabunge baadhi ya

maeneo na vifaa mbalimbali ambavyo vilielekezwa vikabidhiwe na Wabunge, maelekezo haya hayazingatiwi, kwa sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, naomba urejee hayo maelekezo yako ili yasikike. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kumtaka Mkurugenzi Mkuu wa Bohari ya Dawa kuhakikisha kwamba wanashirikiana kwa karibu katika kupeleka au kusambaza vifaa tiba ikiwemo vitanda vya kujifungulia. Wawatafute Wabunge, wapange nao siku, wapeleke mzigo mpaka ngazi ya halmashauri au ngazi ya mkoa, wapange siku na Mbunge na Mbunge ndiyo aseme mimi nitavipokea siku hii na nitakabidhi katika eneo husika. Haya ni maelekezo ya Serikali, yazingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wewe, siyo tu vitanda vya kujifungulia, lakini pia tulinunua vitu mbalimbali ikiwemo magodoro, ikiwemo *ultrasound*, ikiwemo *x–ray machine*. Suala hili naomba nirudi ofisini kulikazia tena. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Serikali inawajibika kwa wananchi kupitia Wabunge, kwa hiyo ni lazima tuhakikishe ushiriki wa Wabunge katika masuala mbalimbali ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ikiwemo katika sekta ya afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mbali na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, mimi nina ombi kutoka Jimbo la Sumve.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Sumve mpaka ninavyoongea hivi tuna majengo ya kuhifadhia maiti katika vituo vya afya vinne ambavyo vimejengwa, lakini yote hayafanyi kazi kwa sababu hayana majokofu.

Je, ni lini Serikali itatuletea majokofu ya kuhifadhia maiti katika vituo vya afya vya Jimbo la Sumve hasa Kituo cha Afya cha Kadashi ili kupunguza adha ya wananchi kwenda katika Wilaya ya Magu kwa ajili ya kuhifadhi wapendwa wao wanapokuwa wamefariki? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Kasalali kwa swali lake zuri la nyongeza kuhusu upatikanaji wa huduma za kuhifadhi maiti katika vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo Mheshimiwa Mbunge ningependa tulisisitize ni kuweka katika mahitaji ya vituo husika kwamba tunahitaji majokofu, wasisubiri labda mpango binafsi wa kupelekewa majokofu. Katika fedha zao zile za dawa, vifaa na vifaa tiba, wanapaswa kuagiza majokofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nilichukue, nitaenda kuangalia pia katika bajeti ya Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama kuna fungu mahsusi la majokofu, lakini wasisubiri, ni hela zao zilezile za dawa, ndiyo maana lile fungu linaitwa dawa, vifaa na vifaa tiba. Kwa hiyo, wataangalia uhitaji wao na ninawashauri waweke kipaumbele katika kununua majokofu, lakini na sisi tutatafuta fedha ya nyongeza kwa ajili hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benardeta Mushashu, swali la nyongeza.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni lini Serikali sasa itajenga jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mama Benardeta Mushashu kwa swali lake zuri. Ni lini? Naomba nisiseme uongo kwa sababu sina uhakika kwenye bajeti hii kama tumetenga fedha za jengo la mama na mtoto, lakini

kubwa Mama Mushashu ambalo umekuwa ukilisisitiza ni kujenga hospitali au kituo kwa ajili ya kuhudumia magonjwa haya ya dharura yanayoambukiza, hiyo tumeiweka kwenye bajeti na nakupongeza sana kwa kupigania Mkoa wa Kagera kuwa na kituo mahsusi cha kuhudumia magonjwa ya dharura kwa sababu kiko mipakani, ni rahisi kupata magonjwa haya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa, kwanza naipongeza Serikali kwa ununuzi wa vitanda, lakini naomba kufahamu kama wamezingatia ununuzi wa *adjustable beds,* ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Stella Ikupa kwa jinsi anavyoweka msisitizo na kufwatilia upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watu wenye ulemavu ikiwemo huduma za uzazi. Tumeanza kununua vitanda ambavyo kidogo viko *adjustable,* lakini nataka kukiri, hatujanunua vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba tulichukue kama suala la muhimu la kufanyia kazi angalau katika kila kituo kinachotoa huduma za uzazi, basi angalau kuweka kitanda kimoja kwa ajili ya huduma za akina mama wenye ulemavu. Tunafahamu changamoto hiyo ipo, lakini naomba sasa tuipe kipaumbele baada ya kujibu swali hili, tutaenda kuifuatilia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Tunduru haina kabisa vifaa tiba vya kuwasaidia watoto njiti, je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba vya kuwasaidia watoto njiti wanaozaliwa

Wilaya ya Tunduru katika Hospitali ile ya Wilaya ya Tunduru? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Hassan Kungu kwa swali lake zuri. Katika bajeti yetu ambayo tumepitisha Bungeni mwezi uliopita, kipaumbele kikubwa katika kuboresha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, ni huduma kwa watoto wachanga ikiwemo watoto njiti. Kwa hiyo, tunategemea, tumepanga fedha za kununua vifaa tiba kwa watoto wachanga na watoto njiti na kuvisambaza katika hospitali zote za wilaya na baadhi ya vituo vya afya jumla 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni eneo ambalo Mheshimiwa Rais Samia ameelekeza kabisa angependa kuona msisitizo tukiboresha zaidi ili kuokoa vifo vya watoto wachanga kuepukana na mambo ya mtoto si riziki. Hayo mambo yamepitwa na wakati, mtoto akiwa njiti, mtoto akiwa mchanga, anaweza kuishi endapo atapata huduma bora mara tu akizaliwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Muhongo, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ni kwamba kuna upungufu wa wafanyakazi wa sekta za afya wengi na bahati sisi Mkoa wa Mara, tuna hospitali kubwa sana yenye jina la Mwalimu. Tumekaa, tumeongea na tumependekeza kwamba kile Chuo Kikuu cha Mwalimu ambacho Makao Makuu ni Butiama, lakini hospitali kubwa iko Musoma Mjini pale kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukasema tuanzishe *Faculty* ya *Medicine*, wataita jina lolote, *school*, sijui *faculty*, ili tupate madaktari, tupate wauguzi, tupate na ma-*nurse* na kwa kuanzia, tuanzie na hizi taaluma ndogo ndogo kama *nurse* na wauguzi, baadaye tutaingia kwenye *medicine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwongezee tu Mheshimiwa Waziri ni kwamba duniani kote, hospitali kubwa zinazofanya kazi kubwa, ni hospitali zile zinatibu na kufundisha na kufanya utafiti yaani *teaching hospitals*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ile ya Mkoa wa Mara, tunataka iwe *teaching hospital* na tunamwomba Mheshimiwa Waziri, hiyo kozi ianze mwakani, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo kwa swali lake zuri na tumelijadili hili suala la kuhakikisha kwamba tunaongeza ufanisi, utendaji na uwezo wa Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Musoma kwa kuipatia Chuo cha Mafunzo ya Afya. Tayari jambo hili pia nimejadili na Mheshimiwa Waziri wetu wa Elimu Mheshimiwa Profesa Mkenda amelibariki na tumeshapata chuo ambacho kiko tayari kwenda kufungua tawi pale Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafanya hivi pia Mheshimiwa Profesa Muhongo, siyo tu kwa sababu ya kutaka kupeleka chuo, lakini tunajiona kama Serikali tunao wajibu wa kuendelea kuthamini na kuenzi kazi kubwa na nzuri ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa hiyo, chuo hiki tutaweza kukijenga pale na nakubaliana na wewe kabisa huduma za afya zinaenda sambamba na tiba, mafunzo pamoja na tafiti. Kwa hiyo hili ni jambo ambalo tutaendelea kulisisitiza katika hospitali zetu zote kubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anastazia James Wambura.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika Hospitali ya Kanda ya Kusini iliyoko Mitengo Mtwara, watoto wanapozaliwa njiti, huwa wanapelekwa katika Hospitali ya Rufaa ya Ligula, lakini pale katika Hospitali ya Kanda ya Kusini kuna michoro kwa ajili ya jengo la mama na mtoto.

Je, ni lini Serikali itajenga jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Ligula? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Anastazia Wambura kwa swali lake na niseme kwa kweli amekuwa akifuatilia sana maendeleo ya Hospitali yetu ya Rufaa ya Kanda ya Kusini. Katika bajeti hii ambayo tumeipitisha ya 2024/2025 moja ya jengo ambalo tutaenda kuliendeleza, ni ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini, kwa hiyo suala hili tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelekezo ya haraka, hatuwezi kuwa na Hospitali ya Rufaa ya Kanda, halafu hawana huduma kwa ajili ya watoto wachanga na watoto njiti. Kwa hiyo, namwelekeza Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini, ndani ya wiki mbili kuweka huduma zote muhimu kwa ajili ya watoto wachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hai-*cost* gharama kubwa, kwa hiyo, anaweza akatafuta chumba kidogo, akaweka vifaa muhimu ikiwemo *phototherapy machine* na vifaa vingine muhimu kwa ajili ya huduma za kusaidia watoto kupumua. Kwa hiyo, naomba hili nilisisitize ndani ya wiki mbili, huduma kwa watoto wachanga, zipatikane katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kusini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako ya ufasaha kwa Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge…

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jambo la Dharura, Jambo la Dharura.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumehitimisha…

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jambo la Dharura, Jambo la Dharura.

**MWENYEKITI:** …maswali.

Matangazo ya wageni na kwanza tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi ambaye ni Afisa Elimu Taaluma kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda ambaye ni Mchungaji wa Kanisa la *Reality of Christ Ministry*, kutoka Sinza Mori, Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Anastazia James Wambura ambao ni Kikundi cha Maendeleo ya Wanawake kutoka mikoa mbalimbali nchini, karibuni sana kama mpo, ndiyo, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni kumi wa Mheshimiwa Joseph Kamonga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Ludewa Mkoa wa Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata ambao ni Machifu kutoka Mkoa wa Rukwa, karibuni sana machifu. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Robert Chacha Maboto ambao ni watumishi kutoka *Maboto Microfinance Company Limited*, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunalo kundi la pili la wageni ambao ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao Ndugu James Issa Dihigo na Ndugu Novia Mazima kutoka Jijini Mwanza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Kezia Claresa Malalo kutoka Kimara Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Irene John Swai kutoka *Mbezi Beach* – Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Ndugu Rodney Damian Kaijanante, Ndugu Alistidia Damian Kaijanante na Ndugu Emmanuel Uswege kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 24 ambao ni wahitimu wa Chuo cha Ualimu Kasulu, karibuni sana na hawa ni wageni wetu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 121 na walimu kumi kutoka Shule ya Awali na Msingi ya Nyamata ya Jijini ya Dar es Salaam, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 17 ambao ni vijana walioteuliwa kushiriki Mafunzo ya Uongozi na Biashara ya *Nelson Mandela Washington Fellowship* nchini Marekani kwa mwaka 2024 wakiongozwa na Ndugu Joseph Malekela, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunayo matangazo mengine muhimu, Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kuwa tarehe 10 Juni, kwa maana ya leo mara baada ya shughuli za Bunge kusitishwa kutakuwa na semina kuhusu masuala muhimu ya kimaadili ya kuzingatiwa na Waheshimiwa Wabunge katika kutekeleza shughuli za Kibunge.

Semina hii itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa, mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge leo. Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria semina hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kuna tangazo muhimu, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa matokeo ya mechi iliyofanyika tarehe 8 Juni, 2024 kati ya timu ya mpira wa miguu ya *Bunge Sports Club* na *Makambako Veterans*, ni kama ifuatavyo; timu ya *Bunge Sports Club* ilipata goli moja na timu ya *Makambako Veterans* ilipata goli moja. *(Makofi)*

Natumia fursa hii kuwapongeza sana *Bunge Sports Club* na *Makambako Veterans*, kwa mechi hii nzuri, lakini nawapongeza

sana *Makambako Veterans*, kwa kujenga urafiki na Bunge na nawaalika wadau wengine wa michezo nchini, waweze kushirikiana na *Bunge Sports Club* kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na kukomazana misuli. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya Jumanne, tarehe 11 Juni saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 5.26 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 11 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*